**MAHUJAJI** Zanzibar waomba serikali iwasaidie Dola



UKURASA 17

**TMDA**, Polisi wanasa dawa, vipodozi hatari zilizofichwa madukani

UKURASA 3



**RC** aipa DART wiki mbili mabasi 70 yarudi barabarani


UKURASA 3

SUPA JACKPOT
TZS.1,161,795,478
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Nipashe
Ijumaa Oktoba 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581462
www.ippmedia.com
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Kashfa nzito TRA

**MFANYABIASHARA** adai ina mfumo wa kuchepusha makusanyo, alia kutozwa Mil. 960/-, yenyewe yajibu... *Endelea ukurasa wa 2*



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA UMMA
Kuhusu Madai ya Bw. Emmanuel Gadi Mmiliki wa Kampuni ya Wintech Tanzania Ltd.

Dar es Salaam, 11 Oktoba, 2023:
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kutoa ufafanuzi juu ya taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu malalamiko ya Bw. Emmanuel Gadi kuwa, TRA imetengeneza mfumo wa kuingiza mizigo nchini nje ya mfumo halali wa Serikali kinyume na Sheria ya Forodha.

Tunapenda kuufahamisha umma na jamii kwa ujumla kuwa, Mamlaka haina mfumo wowote mwingine inaoundesha wa kuingiza mizigo nchini nje ya mfumo wa Forodha wa TANCIS ambao unatumika kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACCMA).

Bw Emmanuel Gadi alifikisha malalamiko yake kwa njia ya barua tarehe 27 Februari, 2023 akidai kupewa uthibitisho na TRA wa kuingiza mzigo wa vifurushi 471 vya "Toner Cartridges" kupitia kampuni ya Tosh Logistics Ltd. TRA ilifanya uchunguzi wa kutosha na kuthibitisha kwamba, hapakuwa na mzigo wowote ulioingizwa nchini kwa jina la Wintech ... vifurushi 471 vya "Toner Cartridges" kupitia kadhia yenye ... tarehe 18 Agosti 2022 kama anavyodai.

...ivyo, TRA ilimjibu ...



Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata

# Kicheko uzalishaji wa dawa nchini, bei kuwa mteremko

UKURASA 2

UKURASA WA 11



Hili la urasimishaji ardhi jamani ugumu uko wapi?
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
SIKU YA MBOLEA DUNIANI... Ruzuku ya TFRA yaleta mapinduzi shambani, Shilingi Bilioni 150 yaletea majibu shambani
MAADHIMISHO MIAKA 24 BILA NYERERE...
Rais Samia anavyotumikia maagizo ya kudumu 'ujinga, umasikini, maradhi' kwa mahitaji ya leo

UKURASA WA 23

## STARS YAELEKEA SAUDI ARABIA KUIVAA SUDAN

KIKOSI cha Timu ya Soka la Taifa (Taifa Stars) kinaondoka nchini leo kuelekea Saudi Arabia kwa ajili ya mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Sudan, imefahamika.

UKURASA WA 24

## SIMBA SC: HATUWAANGUSHI

WAKATI Simba ikizindua rasmi jezi mpya zitakazotumika katika mashindano ya Africa Football League, uongozi wa Wekundu wa Msimbazi umesema kikosi..



## Israel yaitifua Gaza, mabomu yachimbua ardhi

UKURASA 19

**MICHEZO** AZAM YAIREJESHA YANGA 'DARASANI' UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa CCM, Jokate Mwegelo (kushoto), akisalimiana na baadhi ya viongozi wa umoja huo, walipomkaribisha Ofisi za Makao makuu ya UWT, jijini Dodoma jana kwa mara ya kwanza tangu kuteuliwa kushika nafasi hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mfanyabiashara aibua kashfa nzito TRA

**Na Joseph Mwendapole**

MFANYABIASHARA Emmanuel Gadi ameibua tuhuma nzito dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Anashauri Rais Samia Suluhu Hassan achukue hatua kwa madai kuwa mamlaka hiyo imetengeneza mfumo wa kuingiza mizigo nje ya mfumo wa serikali.

Hata hivyo, uongozi wa TRA umekanusha madai ya mfanyabiashara huyo, ikisisitiza haina mfumo mwingine unaoendesha wa kuingiza mizigo nje ya mfumo wa Forodha wa TANCIS.

"Tunapenda kuufahamisha umma kuwa TRA haina mfumo wowote mwingine zaidi ya mfumo uliopo wa TANCIS ambao unatumika kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACCMA), alisema Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Stephen Kauzeni alipofafanua suala hilo jana.

Kupitia ujumbe wa video fupi iliyosambaa katika mitandao ya kijamii jana, mfanyabiashara huyo anadai mfumo huo ulianza kutumika mwaka 2018 (miaka mitano iliyopita). Anadai unafanana na ule uliotengenezwa na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mkoani Mbeya.

Mfanyabiashara huyo anadai TRA ilitengeneza mfumo huo kwa makusudi ili ikusanye mapato kwa maslahi binafsi ya baadhi ya watu na kuisababishia serikali hasara ya mabilioni ya shilingi ambazo zinaingia kwenye mifuko ya watu binafsi.

"TRA wanaacha kodi ya karibu Sh. milioni 400 kutokana na kuficha makosa yao na wananisababishia mimi hasara ya Sh. milioni 968 kwa ajili ya kuficha makosa yao. Ninaomba nirekebishiwe nyaraka zangu ili nilipe ushuru unaostahili wa Sh. milioni 400 ambao niko tayari kulipa," anasema.

Gadi anadai kuwa tangu mwaka 2018, mfumo huo ambao anautaja uko kinyume cha Sheria za Forodha, umekuwa unalazimisha wafanyabiashara kuingiza nchini mizigo kwa jina la wakala, jambo ambalo ni kinyume cha Sheria za Forodha.

Anadai kuwa: "Mwaka jana kampuni ya Tosh Logistic Ltd iliingiza mizigo kwa utaratibu huohuo ambao TRA waliutengeneza na baadaye walibaini kwamba utaratibu ule unakwenda kinyume cha Sheria za Forodha.

"TRA wametoa vibali kwa kampuni mbili kuingiza mizigo ya wafanyabiashara kwa majina ya kampuni zao. Kampuni hizo ni Tosh Logistics na Opo Agency, jambo ambalo halikubaliki kwa mujibu wa Sheria za Forodha," anadai.

Mfanyabiashara huyo anadai kuwa mwaka jana aliagiza mizigo kupitia kampuni ya Tosh Logistics na baada ya mzigo kufika kwenye ghala lao Mkuranga, mzigo huo ulipata ajali ya kuungua hivyo kulazimika kupeleka madai kwenye bima ambayo iliomba nyaraka zilizotumika kuingiza mzigo huo ili walipe fidia.

"Uchunguzi wa kina ulifanyika kuhusu ile ajali na baada ya kukamilika, bima ilituomba nyaraka tulizotumia kuingiza mzigo na mimi nikaenda kwa wakala wangu Tosh Logistics, lakini alikataa, akasema hawezi kuzitoa kwa sababu kuna utaratibu mwingine," anadai.

Gadi anaendelea kudai kuwa Wakala Tosh Logistics aliiandikia kampuni ya bima kuhusu namna mzigo huo ulivyoingia nchini na baada ya kampuni ya bima kupokea barua kutoka Tosh Logistics haikuridhika na taratibu zilizotumika kuingiza mzigo huo na matatizo yalianzia hapo.

"Baada ya kuona hivyo, mimi na kampuni ya bima tuliiandikia barua TRA kuomba ufafanuzi kuhusu utaratibu uliotumika kuingiza mizigo yangu nchini. Cha kushangaza TRA walipokiona kibali chao wenyewe walitamani kukimbia, lakini baada ya siku mbili walianza kufanya uchunguzi," anadai.

Gadi anadai kuwa baada ya siku kadhaa, TRA ilitangaza kuwakumbusha wananchi kuhusu Sheria za Forodha na aliambiwa atulie kwa kuwa kuna utaratibu unafanyika ili apewe fedha zake na Wizara ya Viwanda na Biashara.

"Jambo hili lilinishtua sana, kwamba nipewe fedha zangu na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa msingi upi? Nikaona kweli kuna kitu, nikatulia kidogo wakati ule mgogoro wa Kariakoo uliibuka mara tu walipotangaza zile Sheria za Forodha," anasema.

Anaeleza kuwa kwa kawaida TRA huwa wanajibu barua za wafanyabiashara ndani ya wiki moja, lakini barua yake ilikaa zaidi ya miezi mitano bila kupata majibu. Anadai huenda walikuwa wanajiuliza cha kumjibu kwa kuwa makosa yalikuwa upande wao.

"Baada ya muda mrefu walinijibu lakini namna walivyonijibu hata mtoto mdogo anaweza kugundua kuwa kuna shida kubwa. Nilikutana na ofisa wao mmoja ofisini kwao akaniambia 'suala hili ni gumu na lilipofikia, lazima mmoja wetu aumie, akasema hapa lazima uumie wewe au TRA'. Mimi nikamwambia siwezi kuumia kwa sababu hakuna tatizo nililolitengeneza," anadai.

"Nilimwambia kwamba TRA ndio mlimpa wakala mamlaka ya kuingiza bidhaa zetu kwa jina lake, jambo ambalo ni kinyume cha sheria na ile kampuni ya bima imeng'ang'ania hapohapo na ninavyoowaona TRA wako katika mpango wa kunipotezea nisilipwe Sh. milioni 968 zangu ninaomba Mheshimiwa Rais unisaidie," anasema.

**UFAFANUZI TRA**

Katika ufafanuzi wake jana, Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Kauzeni alidai Gadi alifikisha malalamiko yake kwa njia ya barua tarehe 27 Februari mwaka huu, akidai kupewa uthibitisho na TRA wa kuingiza mzigo wa vifurushi 471 vya Toner Cartridges kupitia kampuni ya Tosh Logistics Ltd.

Alisema TRA ilifanya uchunguzi wa kutosha na kuthibitisha hapakuwa na mzigo wowote ulioingizwa nchini kwa jina la Wintech Tanzania Ltd wa vifurushi 471 vya Toner Cartridges kupitia kadhia yenye namba TZDL - 22-1382193 ya tarehe 18 Agosti 2022 kama anavyodai.

Alisema TRA ilimjibu mhusika kupitia barua yenye kumbukumbu namba CF 8/92/01 ya tarehe 25 Julai 2023, ikimjulisha kuwa kutokana na kukosekana ushahidi wa House Bill of Lading na kutoonekana mzigo huo kwenye kadhia iliyowasilishwa na kampuni ya Tosh Logistics Ltd, TRA isingeweza kuthibitisha kuingizwa kwa mzigo huo nchini.

"Kupitia taarifa ya Emmanuel Gadi aliyoitoa kwenye vyombo vya habari, tumebaini kuwapo kwa viashiria vya ukwepaji kodi kwani ni dhahiri kuwa mzigo wake uliingizwa kwa njia za magendo," alisema Meneja Kauzeni.

Alimtaka mlalamikaji kuwasilisha nyaraka na uthibitisho wa kampuni yake kuingiza mzigo huo nchini mara moja ili hatua stahiki zichukuliwe.

# Kicheko uzalishaji wa dawa nchini, bei kuwa mteremko

**Na Gwamaka Alipipi**

BEI za dawa zinatarajiwa kushuka huku wananchi wakinufaika na uamuzi wa serikali kuingia makubaliano na kampuni za kutengeneza dawa kutoka India, kujenga viwanda hivyo nchini.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alitangaza neema hiyo jana Ikulu jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

"Niwape taarifa njema Watanzania kwamba bei ya dawa inakwenda kushuka. Kinachofanya dawa kuuzwa bei ya juu ni gharama ya usafirishaji. Sasa tunakwenda kujenga kiwanda hapahapa nchini," alisema.

Waziri Ummy alisema kiwango cha dawa kinachozalishwa Tanzania ni kidogo kulinganisha na mahitaji. Asilimia 80 ya dawa hununuliwa nje ya nchi. Kati yake, asilimia 60 hutoka India.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, katika mazungumzo yaliyofanywa kati ya Wizara ya Afya ya Tanzania na India wakati wa ziara hiyo kulisisitizwa umuhimu wa wafamasia wa India kuja nchini kuzalisha dawa.

Alisema kujengwa kiwanda hicho kutawezesha dawa kupatikana kwa wakati, akitolea mfano kwamba hivi sasa uagizaji dawa unachukua takribani miezi tisa kufika nchini kutokana na athari za UVIKO-19.

Waziri Ummy alisema hatua hiyo ikifanikiwa italinufaisha pia soko la Afrika Mashariki pamoja na nchi za Kusini mwa Afrika.

**UPANDIKIZAJI INI**

Waziri huyo pia alisema tayari India imekuwa inashirikiana na Tanzania kutoa huduma bobezi ikiwamo kupandikiza figo na uloto. Sasa kumekuwa na majadiliano ya kuwajengea uwezo wataalamu wa Tanzania kufanya upandikizaji ini.

"Tunao madaktari wabobezi wa kupandikiza ini, lakini watakuja wataalamu kutoka India ambao watawajengea uwezo zaidi. Ndani ya miaka miwili kutoka sasa huduma hiyo itaanza kutolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili," alisema Ummy.

Waziri Ummy pia alisema Hospitali ya Apolo ya India imekubali ombi la Serikali ya Tanzania la kufungua tawi nchini. Badala ya kwenda India, wagonjwa wanasogezewa huduma za afya nchini. Pia alisema Tanzania na India zimekubaliana kuanzisha kituo cha tiba asilia kitakachojengwa eneo la Mkuranga, tayari serikali imeshatenga hekari zaidi ya 100 kwa ajili ya kupanda miti katika eneo hilo.

Waziri Ummy alisema: "Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha tiba utalii, tunataka kuifungua Tanzania iweze kutoa huduma bora katika Afrika. Kwa mfano, mwaka jana tulipokea wagonjwa 6,472 kutoka Comoro, Zambia, Kenya, Malawi."

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali imetenga eneo la hekari zaidi ya 1,000 wilayani Mkuranga mkoani Pwani kwa ajili ya ujenzi wa viwanda 200 vya kampuni za India, baadhi vitazalisha zana za kilimo na dawa za binadamu.

Bashe alisema eneo hilo litakuwa maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya sekta mbalimbali ikiwamo kilimo. Ni sehemu ya makubaliano waliyoingia.

Bashe pia alisema kuwa katika ziara hiyo, Serikali ya Tanzania iliwasilisha mahitaji kwa Serikali ya India kupitia Benki ya Exim ya India kwa ajili ya mradi mkubwa wa umwagiliaji unaotumia maji ya Ziwa Victoria.

Alisema mahitaji hayo ni takribani Dola za Marekani bilioni moja. Mradi huo utatekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Singida, Dodoma, Kagera na Mara.

## HABARI KITAIFA

# Dawa, vipodozi vyenye sumu vyanaswa vikiuzwa kinyemela

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga kwa kishirikiana na Mamlaka ya dawa na Vifaa tiba Tanzania (TMDA), limekamata dawa, vifaa tiba na vipodozi vyenye viambata sumu vikiuzwa kwenye maduka ya dawa bila kibali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Janeth Magomi, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu msako uliofanyika ndani ya mwezi mmoja uliopita.

Alisema, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na TMDA, maofisa afya na biashara mkoani hapa, walikamata dawa ambazo zilikuwa zikiuzwa holela katika maduka ya dawa ya watu binafsi pamoja na vipondozi vyenye viambata sumu vilivyopigwa marufuku.

"Tumekamata dawa za binadamu mchanganyiko ambazo hazina uhalali wametoa wapi kwa sababu hawana nyaraka kuwa wamenunulia wapi zikiwamo sindano, mipira na chupa za dripu na vipodozi vyenye viambata sumu,"alisema.

Kamanda magomi aliongeza kuwa katika msako huo pia walikamata viroba vitano vya mifuko ya plastiki ambayo imepigwa marufuku, mirugi mabunda 20, bangi gramu 1,800, lita tano za gongo na pikipiki sita ambazo zilikuwa zikitumika katika uhalifu na kwamba watu 25 wanashikilia kwa tuhuma mbalimbali.

Pia alisema katika operesheni ya usalama barabarani wamekamata magari 2,331 kutokana na makosa mbalimbali yakiwamo 993 mabovu, 242 kuzidisha abiria, 260 mwendokasi, 179 kutokuwa na bima, 150 mwendo hatarishi na pikipiki na bajaji 749.

Katika hatua nyingine, Kamanda magomi alisema Jeshi la Polisi katika kipindi hicho, liliwafikisha mahakamani watu kwa tuhuma mbalimbali wakiwamo wa ulawiti na ubakaji ambao baadhi yao wamefungwa jela miaka 30 na wengine Maisha.

Aidha, alisema kulikuwa na kesi mbili za wizi wa watoto ambazo wahusika walifikishwa mahakamani na kufungwa miaka mitano jela na mwingine miaka mitatu. Pia mwingine alifikishwa mahakamani kwa kesi ya wizi wa mifugo na amehukumiwa kuitumikia jamii kwa mwaka mmoja.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, ACP Janeth Magomi akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, baadhi ya dawa za binadamu, vifaa tiba na vipodozi vyenye viambata sumu walivyovikamata kwa kushirikiana na Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba Tanzania (TMDA), vikiuzwa kiholela katika maduka ya dawa ya watu binafsi, wakati wa msako walioufanya kwa mwezi mmoja uliopita. **PICHA: MARCO MADUHU**

# RC aipa DART wiki mbili mabasi yarudi barabarani

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ametoa wiki mbili kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuyarejesha barabarani mabasi 70 ambayo yameharibika baada ya matengenezo.

Chalamila ametoa kauli hiyo ikiwa ni siku moja baada ya Nipashe katika ukurasa wake wa mbele jana, kuweka picha ikionyesha adha ya abiria wanayopata katika kituo cha Kimara Mwisho, huku mabasi mengine saba yakiwa yameegeshwa pembeni.

Katika ziara aliyoifanya jana kituoni hapo, Chalamila aliiagiza DART kuhakikisha ndani ya siku 14, mabasi hayo 70 yaliyoharibika yanatengenezwa na kurejea barabarani.

Alisema anashangaa kuona kwa nini idadi kubwa ya mabasi ni mabovu wakati mtoa huduma amekuwa akilipwa fedha katika mradi huo.

Mkuu wa mkoa alisema hatakubali kuona Rais Samia Suluhu Hassan, mwenye nia njema na mradi huo, anatukanwa kwa sababu ya uzembe wa watu fulani kushindwa kutimiza majukumu yao.

Chalamila alisema ndani ya wiki nzima atafanya ziara asubuhi katika vituo vya mradi huo ili kukagua hali ya usafiri.

"Ninawaomba wananchi kuwa na subira kwa kuwa, mchakato wa kuyaleta mabasi bado unaendelea," aliomba.

Baadhi ya abiria wakizungumza na Nipashe jana kuhusu uendeshaji wa mradi huo, waliomba ufanyiwe maboresho zaidi ili kuondokana na changamoto ya abiria kukaa muda mrefu vituoni.


Mkazi wa Mbezi Mwisho, Pendo Adam alisema moja ya maboresho ni kuhakikisha mabasi yanapofika kituoni huko kukiwa na idadi kubwa ya abiria, badala ya kuegeshwa pembeni, madereva wawe wanawabeba.

"Hakuna kitu kinachosha kama unafika kituoni unalazimishwa kupanga foleni muda mrefu halafu ukiangalia upande wa pili wa kituo kuna mabasi yameegeshwa na yanaunguruma na madereva wapo ndani, huku abiria tumejazana kituoni.

"Alafu ukipanda kwenye basi kwa sababu wanaotoa huduma wanakuwa wachache, mnajikuta mmejazana mpaka mlangoni hii kiafya siyo sawa na hata maana ya mwendokasi inakuwa haipo. Huduma ziboreshwe na ziendane na madhumuni ya kuanzishwa kwa mradi huu," alisema.

Jumanne Saidi, mkazi wa Morocco, alisema kuharibika mabasi 70 si sawa kwa sababu mradi wenyewe unaweza kujiendesha na kukarabati basi linapoharibika kwa kuwa abiria wanaotumia mabasi hayo ni wengi.

Mradi wa mwendokasi ulianza mwaka 2016 ambapo hadi sasa idadi ya mabasi ni 210 hivyo kutokana na changamoto hiyo, yanayofanya kazi ni 140.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
(AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. ....41..... OF 20.23..........

THE REPUBLIC
VERSUS
VS

YOHAN MTWEVE..........1ST ACCUSED PERSON

CLARA MPIGA..........2ND ACCUSED PERASON

To:
Yohana Mtweve & Clara Mpiga t/s Kiwangwa Pump Station
Kiwangwa Pump Station, Kiwangwa Area, Chalinze
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the..17th...... day of ..OCT.............. 20.23... at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this ..20th.... day of .....SEPT.............. 20.23............

..........................................
RESIDENT MAGISTRATE - KIBAHA

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTR OF KIBAHA AT KIBAHA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name..........................................

Signature..........................................

Qualification/Relationship
Date..........................................

BancABC part of atlasmara

# AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-23 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-23 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,466 | 5,985 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,626 | 10,506 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 45,516 | 35,787 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 18,097 | 10,484 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 350 | 89 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 92,216 | 98,183 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 130,210 | 128,621 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 16,622 | 17,660 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,020 | 2,070 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **324,123** | **310,386** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 34,365 | 41,016 |
| 18 | Amana za Wateja | 159,968 | 142,729 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | 8 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,370 | 4,201 |
| 28 | Madeni | 100,789 | 96,250 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **298,491** | **284,205** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **25,632** | **26,181** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 139,306 | 139,306 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 409 | 1,033 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (114,835) | (115,460) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (2,266) | (1,717) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,018 | 3,018 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25,632** | **26,181** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 5,911 | 6,009 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 7,492 | 9,199 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,242 | 6,001 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 7.91% | 8.43% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.57% | 6.83% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 69.19% | 73.27% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 40.17% | 41.44% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 48.70% | 47.21% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 5.76% | 0.00% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 4.43% | 0.00% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-23 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-22 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,850 | 10,161 | 31,509 | 30,327 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,603) | (4,889) | (14,310) | (14,764) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6,246** | **5,271** | **17,199** | **15,563** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 500 | 536 | 1,053 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (956) | - | (1,256) | 1,160 |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,908** | **1,856** | **4,700** | **4,697** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 621 | 266 | 1,548 | 652 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 231 | 304 | 906 | 856 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 1,056 | 1,285 | 2,246 | 3,189 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,188)** | **(8,032)** | **(23,786)** | **(22,524)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,919) | (2,760) | (8,479) | (7,920) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,269) | (5,272) | (15,307) | (14,604) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(490)** | **(369)** | **(2,090)** | **(1,104)** |
| **9** | Tengo la Kodi ya Mapato | (59) | (131) | (176) | (196) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(549)** | **(500)** | **(2,266)** | **(1,300)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(549)** | **(500)** | **(2,266)** | **(1,300)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 170 | 178 | 170 | 178 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.22) | (0.20) | (0.23) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.69% | -0.61% | -0.95% | -0.53% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -8.48% | -7.77% | -11.66% | -6.74% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 100.41% | 112.69% | 108.62% | 111.17% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.39% | 2.92% | 3.11% | 2.87% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-23 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-23 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (490) | (520) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,650 | 1,147 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,589) | (1,462) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 10,587 | (5,844) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (9,729) | 8,186 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (840) | 512 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (774) | 2,394 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (59) | (59) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(1,243)** | **4,355** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (50) | (630) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(50)** | **(630)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 4,539 | 3,199 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **4,539** | **3,199** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 3,246 | 6,924 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 125,159 | 118,235 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **128,405** | **125,159** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(114,427)** | **-** | **-** | **3,018** | **11,746** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (2,266) | - | - | - | **(2,266)** |
| Hisa za upendeleo | 16,352 | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (409) | 409 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **139,306** | **-** | **(117,101)** | **409** | **-** | **3,018** | **25,632** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(99,102)** | **2,162.58** | **-** | **989** | **27,004** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (17,288) | - | - | - | **(17,288)** |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 2,029 | **2,029** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 2,163 | (2,163) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(114,427)** | **-** | **-** | **3,018** | **11,746** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 13-Oct-23 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 13-Oct-23 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 13-Oct-23 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 13-Oct-23 |
| 2 | Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 13-Oct-23 |

HABARI KITAIFA

# Rais Samia kuisuka upya Wizara Mambo ya Nje

**Na Restuta James**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema kazi ya kuisuka upya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaanza mara moja ili iweze kwenda sambamba na mageuzi yaliyopo duniani hivi sasa.

Aidha, amesema ili kuendeleza na kukuza wanadiplomasia mahiri, serikali itaandaa mafunzo maalumu ambayo yatawasaidia vijana mahiri waliopo sekta binafsi na serikalini, watakaopikwa na kupangiwa majukumu kulingana na hitaji la nchi.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akipokea ripoti ya Kamati ya Kutathmini Ufanisi na Utendaji wa wizara hiyo, aliyoiunda Machi, mwaka huu.

Alisema kamati imewasilisha mapendekezo yanayogusa wizara hiyo, sekta mbalimbali na sera pamoja na serikali kwa ujumla ambayo yanahitaji uchambuzi wa kina wa namna ya kuyatekeleza.

Alisema ripoti hiyo itafanyiwa kazi kikamilifu ili kurejesha heshima ya Tanzania katika anga za kidiplomasia na kwamba italazimu kuunda timu nyingine zitakazochakata ripoti hiyo ili kurahisisha utekelezaji wa mapendekezo yake.

"Kazi ndio imeanza sasa ya kuisuka upya Wizara ya Mambo ya Nje. Manguli mliotusaidia kufanya kazi hii (kamati), mjue hamjasalimika, niwaombe tuendelee kushirikiana katika kuisuka upya wizara hii," alisema Rais Samia.

Aliongeza kuwa: "Unatakiwa uchambuzi mwingine wa ndani kwa hiyo Katibu Mkuu Kiongozi tengeneza kikundi chako na wizara muichambue muone mnakwenda kuifanyiakazi namna gani."

Alisema miongoni mwa mambo yaliyozorotesha tija katika wizara hiyo ni ajira za kindugu, panga pangua zisizo za lazima wizarani na kutofanyakazi kwa ushirikiano baina ya watumishi.

"Ubobezi uliokuwapo miaka ya 90 hivi sasa haupo. Unguli umahiri na ushawishi wetu uliokuwa kwenye medani za kidiplomasia umekuwa wa kujikongoja na wa kinyonge sana na kumekuwa na malalamiko kutoka taasisi za kimataifa kuhusu utendaji usioridhisha katika wizara hii," alisema.

Kuhusu kupika wanadiplomasia, Rais Samia alisema anataka ndani ya miaka miwili baada ya kuanza mafunzo, wapatikane wanadiplomasia mahiri 90 hadi 120.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Balozi Hassan Simba Yaya, alisema walihoji viongozi waandamizi serikalini, mabalozi, mawaziri na viongozi wa vyama vya siasa.

Alisema wamebaini changamoto kadhaa zikiwamo kutopitiwa kwa muda mrefu kwa sera ya mambo ya mambo ya nje ya mwaka 2001, kutoeleweka kwa dhana ya diplomasia ya uchumi ndani ya serikali, udhaifu wa muundo wa wizara hiyo, upungufu wa watumishi, uchakavu na uharibifu wa majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi, matumizi hafifu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), utaratibu mbovu wa ajira na wizara kukosa utaratibu wa mafunzo.

SIKU YA AFYA YA MACHO

# Utafiti: Magonjwa yasiyoambukiza yachangia tatizo la macho

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAGONJWA yasiyo ambukiza ukiwamo wa kisukari na shinikizo la juu la damu yametajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la ugonjwa wa macho nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa huduma za tiba Wizara ya Afya, Dk. Mwinyiko Amiri, alisema hayo jana kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya afya ya macho duniani kilichofanyika kitaifa jijini hapa.

Alisema, utafiti uliopita pamoja na taarifa mbalimbali za afya zimeonyesha kuwa kuna ongezeko la magonjwa ya macho hasa yanayosababishwa na yasiyo ya kuambukiza kama kisukari na mengine.

"Kwa mfano idadi ya wagonjwa wa kisukari wanaosumbuliwa na matatizo ya macho imeongezeka kutoka wagonjwa 7,065 mwaka 2021 hadi kufikia wagonjwa 10,612 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 33," alisema Dk. Amiri.

Pia, alisema tatizo la macho linalosababishwa na shinikizo la juu la damu limeongezeka kwa asilimia 31 kutoka wagonjwa 3,800 mwaka 2021 hadi 5,571 mwaka 2022.

"Hii inatukumbusha umuhimu wa kuzingatia mtindo bora wa maisha na kuongeza juhudi katika kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza kama njia ya kupunguza changamoto ya watu wenye shida za macho," alisema.

Kadhalika, alisema mwaka huu wanaendesha utafiti wa hali ya ulemavu wa kutokuona na upungufu wa kuona katika Mkoa wa Dodoma.

Alisema wanaendelea kuhakikisha kuwa utafiti huo unachangia kuboresha huduma za macho na afya ya wananchi kwa ujumla.

"Ingawa kumekuwa na maendeleo makubwa katika miaka ya hivi karibuni kwenye huduma za macho bado kuna maeneo yanahitaji kuendelea kuboreshwa.

"Katika hili wizara kwa kushirikiana na wadau tunaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ili kupunguza mzigo kwa wataalam wa macho na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za macho maeneo mbalimbali nchini, teknolojia hizi zitasaidia sana kuongeza ufanisi na upatikanaji wa huduma za macho," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa wataalamu na wadau kuendelea kushirikiana ili kuimarisha huduma za macho nchini na kuboresha maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Meneja Mpango wa Taifa wa Huduma za Macho, Dk. Bernadetha Shilio, alisema asilimia moja ya Watanzania wana ulemavu wa kutokuona na asilimia tatu wana uoni hafifu.

"Sababu nyingi za ulemavu zinazuilika au kuepukika kwa ujumla asilimia 20 ya wananchi wanakuwa na matatizo mbalimbali ya macho na wanahitaji kufikia huduma za macho kwa upimaji, tiba na ushauri karibu na maeneo yao," alisema Dk. Shilio.

Alisema kwa mwaka huu siku ya afya ya macho ni maalumu kwa waajiri na waajiriwa.


## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

| AGENCY BANKING FEE | |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Bill payment | Free |

**Withdrawal Fees**

| Transaction tiers | BancABC Fees | Government Levy | Total Fees |
|---|---|---|---|
| 0-999 | N/A | - | N/A |
| 1,000-1,999 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000-2,999 | 300 | 11 | 311 |
| 3,000-3,999 | 300 | 19 | 319 |
| 4,000-4,999 | 300 | 39 | 339 |
| 5,000-6,999 | 500 | 70 | 570 |
| 7,000-9,999 | 500 | 88 | 588 |
| 10,000-14,999 | 600 | 224 | 824 |
| 15,000-19,999 | 600 | 427 | 1,027 |
| 20,000-29,999 | 600 | 672 | 1,272 |
| 30,000-39,999 | 700 | 770 | 1,470 |
| 40,000-49,999 | 800 | 1,050 | 1,850 |
| 50,000-99,999 | 900 | 1,435 | 2,335 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 1,771 | 2,771 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 2,058 | 3,158 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 2,450 | 3,650 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 2,870 | 4,070 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 3,640 | 5,640 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 4,480 | 6,480 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 4,970 | 6,970 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 5,264 | 7,264 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 6,230 | 8,230 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 6,580 | 8,880 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 6,580 | 9,080 |
| 3,000,001 na zaidi | N/A | 7,000 | N/A |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi kukabiliana na El-Nino yasilegelege

**KUNA** juhudi kubwa zinazofanyika sehemu mbalimbali za maeneo hasa ya Jiji la Dar es Salaam katika maandalizi ya kukabiliana na mvua ya El-Nino.

Mapema mwezi Agosti, Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) katika utabiri wake ilisema kutakuwa na mvua kubwa ya El-Nino ambayo itasababisha mafuriko na kuleta athari.

Mamlaka hiyo ilitoa tahadhari hiyo na kuwataka wananchi na mamlaka mbalimbali kujiandaa kukabiliana na mvua hiyo.

Wakazi wanaoishi mabondeni wametakiwa kuhama maeneo hayo ili mvua hiyo itakapoanza wasiathirike.

Katika majiji mengi nchini kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira wa utupaji taka ovyo. Kutokana na uzoaji taka kutokuwa endelevu, husababisha wananchi kuzikusanya na kuzibwaga barabarani au kwenye mitaro inayopitisha maji.

Hatari ya kutupa taka kwenye mitaro ni kusababisha izibe na maji ya mvua kushindwa kupita kwenye mitaro hiyo ili kuelekea baharini na badala yake hujaa na kutafuta njia nyingine ambayo ni barabarani na kwenye makazi ya watu.

Pia, lile wimbi la wafanyabiashara wadogo kufanya shughuli zao kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wapita kwa miguu limerudi upya barabarani na wanapomaliza biashara zao taka zinaachwa zikizagaa na nyingine kutupwa kwenye mitaro.

Tahadhari inapotolewa ni lazima watu wazingatie kwasababu madhara ya El-Nino ni makubwa na kwa wale waliowahi kushuhudia mvua hiyo mwaka 1998 wanaelewa jinsi ilivyoleta madhara makubwa.

Barabara nyingi ziliharibika, madaraja yalikatika, miundombinu ya kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ilikosekana kwasababu ya kusombwa na maji.

Tumeona kuna kazi inayoendelea katika baadhi ya barabara ambazo wakati wa mvua hujaa maji kutokana na mifereji kuziba, kuna uzibuaji na uondoaji taka zilizotupwa kwenye mifereji hiyo.

Kazi hiyo ni kuhakikisha mvua itakapoanza maji yaweze kupita kwa urahisi kuelekea baharini. Pamoja na jitihada hizo, lakini taka zinazozolewa zinaachwa pembeni ya mifereji bila kuzolewa.

Wasiwasi wetu ni kuwa kama taka hizo zitaachwa kwa muda mrefu bila kuondolewa na ghafla mvua ikaanza kunyesha itakuwa ni kazi bure kwasababu zitaingia tena kwenye mtaro na kwenda kuziba njia.

Wito wetu kwa wanaofanya kazi hiyo ya kuzibua mifereji, wanapomaliza wasirundike milima ya taka pembeni ya mifereji, wazizoe mara moja ili kuepuka athari.

Kwenye mitaa kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake kudhibiti utupaji taka kwenye mifereji. Mara nyingi yanapotokea majanga yanayosababishwa na mvua, lawana huenda kwa serikali bila kujali wananchi wenyewe wanapaswa kuchukua hatua kabla ya kushusha lawama hizo.

Kazi ya serikali ni kujenga miundombinu itakayowanusuru wanawake kuepukana na majanga kama hayo ya mafuriko. Lakini kinachoshangaza wananchi hao wanaojengewa miundombinu ndio wa kwanza kuiharibu.


Wengine huthubutu kuiba mifuniko ya chuma ambayo imewekwa kutoruhusu uchafu kuingia kwenye njia ya maji.

Baadhi ya watu huiondoa na kutumbukiza viroba vya uchafu, halafu maji yanaposhindwa kupita, huwa wa kwanza kuilaumu serikali kuwa haijali wananchi wake.

Majanga yanayosababishwa na mazingira yanaweza kudhibitiwa kama kutakuwa na ushirikano wa kutosha kati ya wanachi na serikali.

Tahadhari zinapotolewa ni lazima hatua zichukuliwe na kila upande ili kuepuka majanga yanayoweza kusababisha vifo na ukosefu wa makazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Chonde chonde tusikilize kilio cha madaktari, vinginevyo tutaisha

**WASWAHILI** husema ukiona la mgambo likilia jua kuna jambo, panapofuka moshi chini kuna moto.

Nimetumia misemo hii, ikiwa ni baadhi ya ambayo mara nyingi imekuwa ikitumika katika jamii kuasa au kutahadharisha kuwa kuna hatari mbele yetu ambayo si rahisi kumuacha mtu salama, kama si kifo bali ni mateso ya maumivu ya muda mrefu ya maradhi au majereha.

Mara kwa mara, wataalamu wa afya, wakiwemo madaktari bingwa wamekuwa wakipiga kelele kwa jamii kuondokana na mtindo wa maisha bwete ambao takwimu walizo nazo zinaonyesha umeleta madhara makubwa kwa watu kufa, wengine kuugua na kuchangia umasikini kutokana na gharama kubwa za matibabu.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, kila kukicha kumekuwa na staili mpya ya maisha katika jamii ambayo imekuwa ikichangia kuongezeka kwa magonjwa yasioyakuambukiza ambayo yamekuwa janga kubwa katika jamii.

Mwanzoni walisema magonjwa hayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi katika jamii kutokana na ulafi kwa kula lundo la vyakula na watu kutofanya mazoezi kila siku.

Wakati wataalam hao wakipasua vichwa vyao, wamekuja kubaini katika utafiti wao kuwa, janga jingine baya zaidi ni ni mtindo wa kutumia bodaboda kwa ajili ya usafiri wa hapa na pale katika maeneo ya mijini na vijijini.

Wanasema bodaboda zinachangia kuongezeka kwa magonjwa hayo nchini, yakiwemo ya moyo, kisukari, saratani na kupoza kwa sababu ya uvivu tu wa watu wengi kutembea hadi vituo vya daladala kutoka majumbani na kurudi.

Changamoto hiyo inatajwa janga jipya kwa sababu inaendelea kuongezeka kwa kasi ya magonjwa hayo ikilinganishwa na miaka ya nyuma kabla ya usafiri huo kuanza nchini.

Sababu nyingine ni jamii kutozingatia ulaji vyakula kwa afya, ikimaanishwa mlo wa kila siku unatakiwa kuwa wa kiasi, isipokuwa matunda na mbogamboga nyingi.

Unywaji wa pombe unatakiwa uwe wa lita 10 kwa mwaka na si vinginevyo, lakini wengi wao wanakunywa kupita kiasi hata zaidi ya kiwango hicho kwa siku, wiki na hata mwezi.

Hali hiyo ukaliibua Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Nchini (TANCDA) kufanya kikao kazi baina yake, wadau na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam ili wapaze sauti zao kwa jamii ibadili mwenendo wa maisha yao.

Katika kikao kazi wadau waliwakata wahariri kutumia kalamu zao kuelimisha jami kudhibiti magonjwa hayo..

Mbali na magonjwa hayo kuathiri familia nyingi kwa kubaki masikini, madatari hao wanasema yamekuwa tishio kwa nguvu kazi ya taifa kwa sababu badala ya mgonjwa kuwa kazini, anatumia muda mwingi kwenda hospitalini kupata matibabu na nyumbani kulala. Vilevile, familia inatumia muda mwingine kumuuguza mgonjwa kwa kukaa nyumbani na kumpeleka hospitalini kwa daktari kuchunguza maendeleo ya afya yake na kupata matibabu badala ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

Tunaambiwa asilimia 50 ya wagonjwa wa kisukari yanaweza kupona iwapo mgonjwa atagundulika mapema.

Wataalamu hao wanaonya tusipochukua hatua mapema kudhibiti magonjwa hayo, kwa siku za baadaye yatakuwa janga kubwa kwa taifa na familia.

Magonjwa haya ni mapambano yetu wenyewe kwa wenyewe, presha (shinikizo la damu) gharama kwa mwezi ni kati ya Sh. 40,000 hadi 60,000 kwa mwezi, kiwango ambacho ni karibia robo ya mshahara wa mfanyakazi kwa mwezi kwa ajili ya kununua dawa.

Mbali na gharama hizo za dawa, mgonjwa na ndugu wamekuwa wakipoteza muda mwingi kwenda hospitalini kufuatilia matibabu na dawa ambayo yatamsogeza siku za kuishi, kisha kufa baadaye.

Ni habari njema kuwa TCD (Chama Wagonjwa wa Kisukari Tanzania) kinawezesha waandishi kwenda kuandika habari dhidi ya magonjwa hayo katika jamii.

Ifike wakati Serikali isikie kilio cha wadau itunge sheria kudhibiti utengenezaji wa vinywaji kwa kutumia sukari, ikiwa ina dhamira ya dhati ya kupambana na baadhi ya magonjwa hayo kama ilivyofanya kwa magonjwa ya kuambukiza ya maleria, homa ya matumbo, kipindupindu, UKIMWI na mfumo wa kupumua.

## HABARI KITAIFA

# Pinda awataka wananchi Butiama kuchangamkia ujio wa chuo kikuu

**Na Mwandishi Wetu,** BUTIAMA

MKUU wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT), Mizengo Pinda amewasihi wakazi wa Butiama kukipokea chuo hicho kwa mikono miwili.

Pinda ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu alisema hayo juzi alipotembelea chuo hicho kwa mara ya kwanza tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo Oktoba, mwaka jana.

"Naomba niwasihi wakazi wa Butiama, mahusiano yetu sasa yajengwe kwa misingi ya urafiki ili mtoto huyu (chuo) aweze kuzaliwa na afya nzuri. Isije ikatokea baada ya siku chache tangu kuanza kwa chuo matukio ya wizi yakatokea. Kwa hiyo, ukisikia watu wanapanga matukio ya wizi, uje utoe taarifa," alisema.

Pinda alisema ujio wa chuo hicho utaleta mabadiliko makubwa kwa jamii inayokizunguka kutokana na kuwa na wanafunzi 6,000 ambao watahitaji huduma za kijamii kutoka kwenye jamii ya Butiama na hivyo kutoa fursa mbalimbambali za kiuchumi.

"Kwa hiyo wale vijana wajanja wenye maono muanze kuona wanafunzi 6,000 wapo Butiama. Msije mkafikia hatua ya kujilaumu kwa nini nilichelewa au kwa nini sikuliona hili. Mwanzishe migahawa na huduma mbalimbali baada ya kujua wanafunzi wanataka nini. Kubwa ni kwamba, nataka niwatahadharishe muweze kuliona hili msije kujilaumu," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Balozi Philemon Luhanjo, alisema chuo hicho kimeshindwa kufanya udahili wa wanafunzi kwa kipindi cha miaka saba kutokana na kukosekana kwa miundombinu stahiki.

"Msisitizo mkubwa umeelekezwa katika kujenga miundombinu kwa kuanza na ukarabati wa majengo yaliyokuwa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Oswald Mang'ombe. Nipende kuishukuru serikali kwa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha na rasilimali watu kwa ajili ya ukarabati wa kampasi anzilishi ya Oswald Mang'ombe. Ujenzi wa Kampasi Kuu na ujenzi wa Kampasi ya Tabora utaanza hivi karibuni," alisema.

Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT) kinatekeleza mradi wa ukarabati katika kampasi ya Oswald Mang'ombe wenye thamani ya Sh. bilioni 2.661 na Mradi wa Elimu ya Juu Kwa Mageuzi ya Kiuchumi katika Kampasi Kuu Butiama na Kampasi ya Tabora wenye thamani ya Sh. bilioni 102.5.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT), Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda akizungumza na wajumbe wa Baraza la chuo pamoja na watumishi alipofanya ziara ya kwanza chuoni hapo Butiama mkoani Mara, tangu alipoteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo Oktoba, 2022. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wahimizwa mkakati kulisha Afrika

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

WADAU wa kilimo wametakiwa kuwa karibu na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) ili mikakati ya kuzalisha mazao ya kilimo na biashara itekelezwe kwa ufanisi.

Pia, kushirikiana kwa wakulima na SAGCOT kumetajwa kuwa chanzo cha kutimiza ndoto ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuifanya Tanzania kuzalisha chakula cha kulisha bara la Afrika.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alitoa agizo hilo jana kwa wadau wa kilimo katika mkutano wa wadau kutoka taasisi za sekta binafsi na umma zilizoko katika Kongani ya Ihemi.

Alisema kwa kushirikiana na SAGCOT katika kuhamasisha wakulima kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula na biashara, kutasaidia ziada ya mazao ya chakula iwe kubwa na ilishe bara la Afrika ifikapo 2030.

Mtaka alisema kuzalisha ziada kubwa ya chakula kwa kutumia mikakati iliyo, ikiwamo utoaji wa mbolea ya ruzuku ni dhamira ya serikali ya kulisha Afrika ifikapo 2030.

"Kulisha Afrika ni ndoto ya Rais Samia na ni dhamira ya serikali anayoiongoza. Mnaona ameshasema visima 68,000 vichimbwe kwaajili ya umwagiliaji lakini pia mabwawa yachimbwe na pesa zimeshatolewa kwaajili kuanza uchimbaji," alisema Mtaka.

Mkuu wa Maendeleo ya Kongani na Ubia wa SAGCOT, Maria Ijumba, alisema ndani ya mwaka mmoja, limekuwako ongezeko kubwa katika nyanja za ajira, uzalishaji na uwekezaji, kuwa sekta ya kilimo imesaidia kundi kubwa la Watanzania kuushinda umasikini.

Alisema tathimini ya mwaka 2022 inaonyesha kuwa wakulima wadogo wa mazao ya biashara wameongezeka mara nane kutoka 100,000 hadi 847,385.


**MWANGA HAKIKA BANK**

## MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
## MINIMUM DICLOSURE OF CHARGES AND TARIFFS

| PRODUCTS/ SERVICES | BUSINESS CURRENT A/C | PREMIUM CURRENT A/C | PERSONAL SAVING A/C | SALARY A/C | MTOTO SAVING A/C | JIPANGE SAVING A/C | WEKEZA GROUP A/C | MALENGO SAVING A/C | FOREX ACCOUNT USD & EURO | JIWEKEE SAVING A/C | MHB PAMOJA A/C | MSOMI ACCOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening | 100,000.00 | 50,000.00 | 20,000.00 | 0 | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 | 100,000.00 | 10 | 0 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| Minimum operating Balance | 100,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 | 5,000.00 | 5,000.00 | 0 | 10,000.00 | 100,000.00 | 10 | 10,000.00 | 50,000.00 | 5,000.00 |
| Interest Payable | N/A | N/A | 3.00% | 3.00% | 6.00% | 2.00% | 3.00% | 2% < 10Mil, 4%>=10Mil | 0.50% | 2.00% | 2% | 3.00% |
| Interest bearing amount | N/A | N/A | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 | 5,000.00 | 20,000.00 | 500,000.00 | 20,000.00 |
| Monthly Mantainance fee | 20,000.00 | 10,000.00 | 2,500.00 | 2,500.00 | Free | Free | Free | Free | 2 | Free | Free | Free |
| Deposit | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Adhock statement Per page | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 1 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 |

### OTHER CHARGES

| SERVICES | AMOUNT ( TZS) |
|---|---|
| Certificate of Balance | 30,000.00 |
| Confirmation to the Auditors | 30,000.00 |
| Search for information above 5 years | 15,000.00 |
| Cheque book cost (Per Leaf) | 600.00 |
| Status report | 30,000.00 |
| Stop payment order | 30,000.00 |
| Dishonoured cheque for lack of funds or refer to drawer or effect not cleared | 100,000.00 |
| Dishonoured cheque due to the technical error caused by customer | 60,000.00 |
| Dormant Account Activation | Free |
| Account Closing on Customer Demand | 10,000.00 |
| Counter cheque per leaf [Within the Bank] | 15,000.00 |
| Salary Processing fee [ per Transaction] | 1,000.00 |
| Customer ID | 10,000.00 |
| Pre-Mature breaking of Fixed Deposit on customer request | Minimum of 50% of the accrued interest |
| CCTV Camera footage searching request from Customer | 30,000.00 |
| Uncollected Cheque Book/Destruction | 5,000.00 |
| Visa Card Issuance-Classic | 10,000.00 |
| Visa Card Issuance-Gold | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Classic | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Gold | 25,000.00 |
| Umoja Card Mantainance fee | 1000 per month |
| Visa Card- Classic Mantainance fee | 3,000 per QTR |
| Visa Card-Gold Mantainance fee | 5,000 per QTR |
| Uncollected ATM Card | 5,000.00 |
| PIN reset fee | 5,000.00 |
| Withdraw fee local (Umoja ATM) | 1000-99,000=1500 100,000-400,000=1700 |
| Withdraw fee other Bank (Domestic Banks) | 3,500 |
| Withdraw fee other Bank (International) | 11,000 |
| Balance inquiry Umoja ATM | 300 |
| Balance inquiry other Domestic Banks | 950 |
| Balance inquiry other Bank (International) | 2,000 |
| Decline Domestic [Insufficient fund] | 1,000 |
| Decline International [Insufficient Balance] | 1,500 |
| QR transactions | 3% of Transaction Amt |
| POS transactions | 3% of Transaction Amt |
| E-commerce transactions | 3% of Transaction Amt |

**Cash Withdraw Over the Counter [TZS/ USD/EURO]**

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Wekeza/Jiwekezee | 2,000.00 |
| Bellow 10 Mil | 3,000.00 |
| Above 10Mill to 50 Mil | 0.10% |
| Above 50Mil t0 100 Mil | 0.090% |
| Above 100Mil to 300 Mil | 0.089% |
| Above 300 Mil | 0.079% |

**Cash Withdraw Over the CounterForeign Currency [USD/EURO]**

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Below USD/EURO 4,000 | 2 |
| Above USD/EURO 4000 | 0.1% more than USD/EURO 40 |

### AGENCY BANKING CHARGES

| TYPE OF SERVICES | RATES |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Balance Inquiry | 500 |
| Min Statement | 700 |
| Transfer of fund within MHB | 2,000 |
| Transfer of funds to other Bank | 13,000 |

### AGENCY BANKING WITHDRAWAL FEE

| AMOUNT | FEE |
|---|---|
| Up to 50,000 | 850.00 |
| 50,000 - 100,000 | 1,000.00 |
| 100,000 - 300,000 | 2,000.00 |
| 300,000 - 500,000 | 3,500.00 |
| 500,000 - 1,000,000 | 4,500.00 |
| 1,000,000 - 3,000,000 | 6,000.00 |
| 3,000,000 - 5,000,000 | 10,000.00 |

### MOBILE BANKING CHARGES

**WITHDRAWAL CHARGES**

| MINIMUM [TZS] | MAXIMUM [TZS] | RATES [TZS] |
|---|---|---|
| 0 | 10,000 | 800 |
| 10,001 | 19,999 | 1,800 |
| 20,000 | 49,999 | 3,500 |
| 50,000 | 99,999 | 5,200 |
| 100,000 | 199,999 | 7,200 |
| 200,000 | 499,999 | 8,200 |
| 500,000 | 999,999 | 10,500 |
| 1,000,000 | 2,000,000 | 11,200 |
| 2,000,001 | 3,000,000 | 12,000 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 15,000 |

**FUND TRANSFER CHARGES**

| | |
|---|---|
| Transfer of Funds within MHB | 2,000.00 |
| Transfer of funds to other Banks | 13,000.00 |

### EFT/SWIFT/TISS

| | |
|---|---|
| EFT within the Bank (Incoming) | Free |
| EFT to other Banks | 1,500.00 |
| TISS Transfer | 10,000.00 |
| T.T. Transfer | - |

### STANDING ORDER

| | |
|---|---|
| Instructions within MHB | FREE |
| Standing Order to other Bank | 10,000/= |

www.mhbbank.co.tz

217643701

# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30/09/2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo mwaka ya 30.09.2023 | Robo mwaka ya 30.06.2023 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha tasilimu | 1,699 | 1,752 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 2,833 | 2,875 |
| 3 | Uwekezaji katika amana serekalini | 0 | 0 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 7,334 | 5,396 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushuhulikiwa | 195 | 201 |
| 6 | Miamala baina ya matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili zililizo afikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za wateja zilizo kubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 35,161 | 35,718 |
| 12 | Mali nyingine | 2,645 | 2,738 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | 35 | 35 |
| 14 | Akauti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali zisizohamishika , mitambo na vifaa | 1,513 | 1,574 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | 51,415 | 50,289 |
| | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | 0 | 0 |
| 18 | Amana za wateja | 36,439 | 36,471 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha tasilimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limbiko za kodi na gharama zitakazolipwa | 357 | 239 |
| 24 | Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala isiyoshuhulikiwa baina ya matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadae | 0 | 0 |
| 27 | Dhima nyingine | 501 | 515 |
| 28 | Madeni | 555 | 555 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **37,852** | **37,780** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 29)** | **13,563** | **12,509** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 11,097 | 10,227 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | 805 | 805 |
| 34 | Faida (hasara) ya kipindi husika | 950 | 765 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 711 | 712 |
| 36 | Stahiki ya mwenye hisa chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **13,563** | **12,509** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | **3,742** | **3,584** |
| 39 | Mikopo chechefu | 2,079 | 1,808 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 758 | 722 |
| 41 | Malinyingine chechefu | 0 | 0 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 26.38% | 24.87% |
| | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 5.75% | 4.95% |
| | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 97.09% | 98.42% |
| | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 68.39% | 71.03% |
| | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 82.65% | 81.76% |
| | Ongezeko la amana | 0.09% | 3.42% |
| | Ongezeko la mali | 2.24% | 3.75% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30/09/2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya mwaka ya sasa 30.09.2023 | Robo ya Mwaka 30.06.2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30.09.2023 | Limbikizo la mwaka Linganishi 30.09.2022 |
|---|---|---|---|---|
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uendeshaji** | | | | |
| **Mapato/(hasara) halisi** | **293** | **300** | **1,232** | **1,080** |
| **Marekebisho kwa ajili ya:-** | - | - | - | - |
| Uchakavu | 103 | 100 | 335 | 337 |
| **Badiliko halisi katika mikopo** | **557** | **(3,087)** | **(4,107)** | **(2,117)** |
| Faida / (hasara) kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika amana | (32) | 1,206 | 3,618 | 890 |
| Mabadiliko katika amana za muda mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 104 | 178 | 96 | 238 |
| Mabadiliko halisi katika mali nyingine | 93 | (440) | (804) | 342 |
| Kodi iliyopitwa | (114) | (114) | (162) | (135) |
| Mengineyo (bainisha) | (37) | 202 | 26 | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uendeshaji** | **967** | **(1,655)** | **234** | **635** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uwekezaji** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa mali za kudumu | - | (22) | (183) | (571) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa amana zisizoshuhulikiwa mawakala | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshuhulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (15) |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uwekezaji** | **-** | **(22)** | **(183)** | **(586)** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za kifedha** | | | | |
| Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Ongezeko la hisa | 870 | 8 | 922 | 974 |
| Gawio lililolipwa kwa fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika madeni mengine | - | - | (112) | (167) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za kifedha** | **870** | **8** | **810** | **807** |
| **Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | | | | |
| **Ongezeko /punguzo katika fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | **1,837** | **(1,669)** | **861** | **856** |
| Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/mwaka | 10,224 | 11,893 | 11,200 | 10,344 |
| **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/mwaka** | **12,061** | **10,224** | **12,061** | **11,200** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO YA MWAKA ULIOISHIA 30.09.2023

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Mr. Samwel A. Wado **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | S. Wado | 13rd Oktoba, 2023 |
| Mrs. Anitha J. Mnkeni **(Idara Ya Fedha)** | A. Mnkeni | 13rd Oktoba, 2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| *" Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1. Mr. Wilson Ndesanjo **(Mwenyekiti wa Bodi)** | W .Ndesanjo | 13rd Oktoba, 2023 |
| 2. Mr. Munguatosha M. Makyao **(Mkurugenzi)** | M.Makyao | 13rd Oktoba, 2023 |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO YA MWAKA UNAOISHIA 30/09/2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka wa sasa 30.09.2023 | Robo ya Mwaka Linganishi 30.09.2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30.09.2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Mapato ya riba** | **1,836** | **1580** | **4,943** | **4,465** |
| 2 | Gharama za riba | 452 | 47 | 1,235 | 860 |
| 3 | Madeni viza yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | **Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **1,349** | **1,450** | **3,589** | **3,522** |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | 35 | 83 | 119 | 83 |
| 6 | **Mapato yasiyo na riba** | **293** | **297** | **1009** | **796** |
| | 6.1 Faida /hasara zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 16 | 25 | 68 | 55 |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 236 | 250 | 860 | 663 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato mengine | 41 | 22 | 81 | 78 |
| 7 | **Gharama zisizo za riba** | **1,349** | **1,182** | **3,576** | **3,238** |
| | 7.1 Mishahara na mafao | 650 | 531 | 1,737 | 1591 |
| | 7.2 Ada na kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama nyingine za uendeshaji | 699 | 651 | 1,839 | 1647 |
| 8 | **Faida/(hasara) ya uendeshaji** | **293** | **565** | **1,022** | **1,080** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | 114 | 45 | 282 | 135 |
| 10 | **Faida/(hasara) halisi baada ya kodi ya mapato** | **179** | **520** | **740** | **945** |
| 11 | Mapato mengine yaliojumuishwa (bainisha) | 6 | 0 | 210 | 0 |
| 12 | **Jumla ya faida /(hasara) iliojumuishwa kwa mwaka** | **185** | **520** | **950** | **945** |
| 13 | idadi ya waajiriwa | 52 | 48 | 52 | 48 |
| 14 | mapato kwa hisa | 1.67% | 5.11% | 8.56% | 9.29% |
| 15 | idadi ya matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | **BAHADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa mali | 0.35% | 1.13% | 1.87% | 2.06% |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa fedha za wanahisa | 1.37% | 4.62% | 5.68% | 8.39% |
| | uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 63.36% | 62.97% | 60.08% | 61.55% |
| | uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani ya mali zinazozalishwa | 3.81% | 4.62% | 10.13% | 11.21% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBE, 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya kwanza inayoanza 01.01.2023** | **10,227** | **17** | **1,017** | **596** | **30** | **68** | **11,955** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato 30.09.2023 | 0 | 0 | 950 | 0 | 0 | 0 | **950** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 870 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **870** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mabadiliko katika tengo la mikopo chechefu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | (211) | 0 | 0 | 0 | **(211)** |
| **Salio la mwisho wa robo ya kwanza ya mwaka 30.09.2023** | **11,097** | **17** | **1,756** | **596** | **30** | **68** | **13,564** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **10,094** | **17** | **(766)** | **1234** | **30** | **100** | **10,709** |
| | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 1,145 | 0 | 0 | 0 | **1,145** |
| Miamala na wanahisa | 115 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **115** |
| Mabadiliko katika tengo la mikopo chechefu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya juu ya hisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 638 | (638) | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | -32 | **(32)** |
| Kodi ya mwaka uliopita | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2022** | **10,209** | **17** | **1,017** | **596** | **30** | **68** | **11,937** |

### REVIEWED CHARGES AS AT 30.09.2023

| | | | |
|---|---|---|---|
| B | **DEPOSIT RATES** | | RATES |
| | Savings Account **(p.a)** | | 1% |
| | Mavuno Account - Special Deposit Account (p.a) | | 9% |
| | **Fixed Deposit** | | |
| | 3 Months | | 4% |
| | 6months | | 5% |
| | 12Months | | 6% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 50Mil | | 6% to 7% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 100Mil | | 8% to 9% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 500Mil | | 10% |
| C | **CHARGES AND FEES** | | |
| | **ITEM/TRANSACTION** | | **CHARGE/FEE** |
| 1 | **Current Accounts** | **USD** | |
| | Minimum Opening balance - Company and individual | 50.00 | 100,000.00 |
| | Monthly Statement enquiry | 2.00 | TZS 1,500 per month and TZS 700 for extra page |
| | Monthly Ledger fee | 10.00 | 15,000.00 |
| | Account closing charges | 10.00 | 20,000.00 |
| | Sale of bankers cheque | | 30,000.00 |
| | Cancelation of bankers cheque | | 30,000.00 |
| | Cheque book per leaf | 0.18 | 400.00 |
| | Stop payment order | 10.00 | 30,000 reported lost/stolen cheque book/leaf (per notice) |
| | Standing order within the bank per entry | 2.00 | 1,000.00 |
| | Standing order to other banks per entry | 20.00 | 15,000.00 |
| | Confirmation of Balance and Audit statement | 25.00 | 50,000.00 |
| | Salary processing fee per entry | N/A | 2,000.00 |
| | Upaid cheque (RD) | 40.00 | 40,000.00 |
| | Montly fees - Parishes Account | N/A | 5,000.00 |
| | - Other Current Account | N/A | 15,000.00 |
| | Quartely fees - Other Current account | | 2,000.00 |
| | Deposit fee | N/A | free |
| | Withdrawal on current account using cheque | | Up to TZS 400,000 TZS 1,500, 400,000.001 to 5,000,000 TZS 2,000 from 5,000,000.001 above 0.05% max 150,000 |
| 2 | **Savings Accounts** | | |
| | Minimum Operating Balance | Mavuno Saving Account | 5,000.00 |
| | | Uchumi Account | 10,000.00 |
| | | Personal Saving | 20,000.00 |
| | Account closure | | 20,000.00 |
| | Dormant account reactivation | | free |
| | Withdrawal fee over the counter | 1% of the amount | Up to TZS 400,000 TZS 1,500, from 400,000.001 to 5,000,000, from 5,000,000.001 to 10,000,000 TZS 2,000 from 10,000,000.001 to 50,000,000 TZS 10,000,000 from 50,000,000 TZS 0.05% max TZS 150,000 |
| | Account maintenance fee - Monthly | | 1,500.00 |
| | - Quartely | | 1,600.00 |
| | Bulk Cash deposit | | free |
| | New ATM card issuance | N/A | 10,000.00 |
| | ATM card renewal or replacement | N/A | 15,000.00 |
| | ATM withdrawal fee | | 1,300.00 |
| | PIN Reset ATM | | 5,000.00 |


| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | **Electronic Banking** | | |
| | SWIFT/TISS transfer | | 11,800.00 |
| | Mobile banking balance enquiry | | 200.00 |
| | Transfer from bank account to mobile | | |
| | Mobile - PIN reset | | 2,000.00 |
| | **Other Charges** | | |
| | Cheque clearing fee (Outward Cheques) | | 1,000.00 |
| | EFT | | 2,000.00 |
| | Search fees (including vouchers) | | one month free, 2 to 6 months 20,000, above 6months 50,000. CCTV footage 30,000 max 6months |
| | Uncollected cheque book (after notification) | | TZS 2,000 per month |
| | Coins deposit | | 3% of the deposited amount (non parish) |
| | Brela Search Fees | Company Limited | TZS 25,000 |
| | | Trade name | TZS 7,000 |
| 4 | **Internet Banking** | | |
| | 24/7 Transfer UCB to UCB | | Free |
| | 24/7 Transfer (Other Banks) | | 11,800.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 1,000 -100,000 | 2,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 101,000-200,000 | 3,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 201,000-500,000 | 5,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 500,1000-1,000,000 | 6,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 1,001,000-2,000,000 | 8,500.00 |
| | 24/7 Airtime processing | Payment | free |
| | 24/7 Government payment | | free |
| | 24/7 Other payments (utility) | DSTV, Star Times, AZAM, Water Bills etc. | 1,500.00 |
| | Balance inquiry | | Free |
| | Monthly fee per retail user | | 1,500.00 |
| | Monthly fee for corporate user | | 2,500.00 |
| | Retail & Corporate subsricption | | Free |
| | Bank statement self download | | 500.00 |
| | Cheque book request 100 leaves | | 47,200.00 |
| | Cheque book request 50 leaves | | 23,600.00 |
| | PIN Regeneration | | Free |
| | Salary processing | | 1,800.00 |
| | Standing Order Instructions | | 2,000.00 |
| | **5. Tips Charges** | | |
| | 24/7 Fund Transfer | 1-49,999 | 1,700 |
| | 24/7 Fund Transfer | 50,000-99,999 | 2,600 |
| | 24/7 Fund Transfer | 100,000-299,999 | 3,500 |
| | 24/7 Fund Transfer | 300,000-999,999 | 5,000 |
| | 24/7 Fund Transfer | 1,000,000-1,999,999 | 8,500 |
| | 24/7 Fund Transfer | 2,000,000-2,999,999 | 10,500 |
| | 24/7 Fund Transfer | 3,000,000-Above | 11,800 |
| | 24/7 Fund Transfer | | |

### UCB OFFERS THE FOLLOWING PRODUCTS:

- *Savings Accounts*
- *Current Account*
- *Elimu Juniour Account*
- *Mavuno Savings Account*
- *Uchumi Savings Account*
- *Fixed Deposit Accounts-(FDR) with attractive Rates*
- *Forex Accounts*
- *Bureau De Change*
- *ATMs Services,all over the Country-Umoja Switch*

CARING FOR FAMILY ECONOMY


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422





# Mndeme awataka viongozi kutatua kero za wananchi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amesisitiza uwajibikaji ikiwa ni pamoja na kuwakumbusha majukumu maofisa tarafa, watendaji kata, mitaa na vijiji mkoani humo kuhakikisha wanatatua kero za wananchi, kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ukusanyaji mapato.

Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na watumishi hao na kuwataka kuongeza ufanisi wa utendaji wao kazi katika kuwahudumia wananchi na kuitumikia serikali pia.

"Amkeni mfanye kazi, tatueni kero za wananchi, simamieni miradi ya maendeleo na ukusanyaji mapato, msisubiri kazi hizi kufanywa na viongozi wakubwa haya ni moja ya majukumu yenu," alisema Mndeme.

Aidha, aliwataka watumishi hao kusimamia pia suala la utunzaji wa mazingira katika maeneo yao na kuhakikisha wanadhibiti uharibifu wa mazngira katika namna yoyote.

Katika hatua nyingine Mndeme, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri, kuwalipa stahiki zao watumishi hao kwa wakati, huku akiagiza pia waandaliwe na mafunzo ya utumishi wa umma ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Watumishi hao walimwahidi mkuu wa mkoa kubadili mifumo yao ya kiutendaji na kuhakikisha wanafuata maelekezo yake ili kuaidia hatua ya utoaji huduma kwa wananchi.

# Bashungwa atoa angalizo utoaji zabuni kwa makandarasi

**Na Remmy Moka,** SAUT

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amemwagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kutokutoa tenda nyingine kwa mkandarasi yeyote ambaye anatekeleza mradi ambao haujafikia asilimia 60 ili kuondoa hali ya kumrudikia kazi mkandarasi mmoja.

Waziri Bashungwa alitoa kauli hiyo juzi jijini Mwanza katika ufunguzi wa mkutano wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi uliolenga kuwajengea uwezo wakandarasi wazawa wa kutekeleza miradi kwa wakati.

"Kama kuna wakandarasi wanaotekeleza miradi ya barabara au kazi nyingine ya ujenzi na wako chini ya asilimia 60 msiwape miradi mingine hakikisheni hiyo inaelekea kukamilika ndipo wapewe miradi tofauti na hapo mnawapa wakati mgumu wa kuimaliza kwa wakati," alisema Bashungwa.

Katika hatua nyingine Waziri Bashungwa alisema serikali imejitahidi kulipa madeni ya makandarasi wa ndani baada ya maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuagiza madeni hayo kulipwa.

Vilevile, alisema kuwa kwa yale ambayo bado hayajakamilishwa, serikali itahakikisha inalipa madeni hayo yote ifikapo mwezi Novemba 2023.

Aidha, Waziri Bashungwa alitembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa vivuko vipya vitano vilivyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 20 pamoja na ukarabati wa vingine kikiwamo kivuko cha MV. Mara kilichogharimu zaidi ya Sh.milioni 300 katika karakana na Songoro Marine, wilayani Ilemela.

Alitaja hatua hiyo kuimarisha hali ya usafiri kwa wananchi wanaoishi maeneo ya visiwa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuagiza Kampuni ya Songoro Marine kukamilisha asilimia moja iliyobaki kwenye ukarabati wa Kivuko cha MV. Mara kwa mujibu wa mkataba kufikia Oktoba 15, 2023 ili kikahudumie wananchi kwenye visiwa vya Wilaya ya Musoma.

"Niwatake TASAC kuja kukikagua kwa haraka kivuko hiki ili kikawaondolee adha ya usafiri wananchi wa Mara na kuinua shughuli zao za kiuchumi na kijamii," alisema Waziri Bas

Vilevile, Waziri Bashungwa aliagiza ukamilishaji wa vivuko vya Rugezi- Kisorya (70%), Ijinga- Kihangara (67%), Bwiro- Bukondo (70%), Nyakalilo- Kome (55.5%), Butagu -Mbalika (30%), MV Nyerere na MV Kilombero ili vikawahudumie wananchi na kutimiza adhma ya serikali ya kuboresha huduma za usafiri wa majini.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Amos Makalla alisema ujenzi wa vivuko hivyo unaboresha huduma za usafiri kwa kuhakikisha wananchi wanapata vivuko ambavyo ni bora na salama viwapo majini na kuondoa adha ya ajali za mara kwa mara majini.

Waziri Bashungwa alikagua ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi lenye urefu wa kilomita 3.2 linalojengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 700 na kumwagiza Mkuu wa mkoa kumsimamia mkandarasi anayejenga daraja hilo ili akamilishe kwa wakati.



Mkazi wa Dar es Salaam, Ally Nchahaga (kwenye gari), akipata huduma ya bima kutoka kwa Mtoa huduma wa Total Energies, Celina Chambi alipofika kwenye kituo cha mafuta cha kampuni hiyo, jijini humo jana, akiwa ni mteja wa kwanza baada ya uzinduzi wa kampeni maalum ya Bima Mazima, inayotoa fursa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri hususani wanaoishi Dar kupata huduma mbalimbali za kibima kupitia kampeni hiyo inayoratibiwa na benki ya NBC kwa kushirikiana na Jubillee Allianz. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukosefu wa maji wadaiwa kuvuruga ndoa Kishapu

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa vijiji vinane katika Kata ya Itilima, Halmashauli ya Kishapu mkoani Shinyanga wamelalamikia hali ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu katika vijiji hivyo hatua inayosababisha ndoa zao kuwa na migogoro ya mara kwa mara na wakati mwingine kuvunjika.

Inadaiwa kuwa wanawake katika vijiji hivyo mara kadhaa wanapokea kichapo kutoka kwa waume zao wakituhumiwa kuchelewa kurejea nyumbani wakati wakitafuta maji.

Wananchi hao waliwasilisha malalamiko yao mbele ya Mbunge wa jimbo hilo, Boniface Butondo wakati wa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi na kuiomba serikali kulitazama eneo hilo na kulipatia huduma hiyo muhimu kunusuru ndoa zao na afya kwa ujumla.

Mkazi wa Kijiji cha Ilebelebe, Kata ya Itilima, Regina Kasembe, alisema wanaumwa matumbo mara kwa mara na wanawake ndio wanaoteseka zaidi kutafuta maji, wakitoka usiku wa manane na kurejea majira ya saa mbili ya asubuhi na kuanza kugombezwa na waume zao.

"Shida yetu kubwa ni majisafi na salama, kwani toka uhuru tunakunywa maji yasiyo salama na kuyapata ni mpaka uhangaike tunakuomba kilio hiki kifike kwa Rais tupate maji na sisi ili tupate amani kwenye ndoa na familia zetu," alisema Kasembe.

Mseven Nkuba alisema shida sio maji kuwa mbali bali wanawake wanaacha familia na kutumia muda mwingi kuyafuata hali inayowakosesha unyumba.

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Hamis Kiswala, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kueleza kuwa tayari serikali imetenga fedha kwaajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika kata hiyo kupitia mwaka wa fedha 2023/24 na wanaendelea na taratibu kulingana na bajeti.

"Tunaanza na visima vifupi katika mpango mfupi na mpango wa muda mrefu ni kuhakikisha mnapata maji ya Ziwa Victoria," alisema Kiswala.

Kiswala alisema zaidi ya Shilingi bilioni tatu zitatumika kwa ajili ya kuleta maji katika kijiji cha Ilebelebe Ikoma Ipeja na Itilima hivyo wataanza na vijiji vinne huku wakijiandaa na vijiji vingine.

Mbunge wa jimbo hilo, Boniface Butondo alitoa pole kwa wananchi hao ambao wanaendelea kuteseka kupata maji na kuahidi kuwahangaikia ili kuhakikisha zinapatikana fedha, kata ya Itilima na kata zingine zinapata maji na mkakati uliopo Itilima ipate majisafi na salama.




Ukurasa 13

Hili la urasimishaji ardhi jamani ugumu uko wapi?

# BUFE

IJUMAA OKTOBA 13, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## SIKU YA MBOLEA DUNIANI... Nguvu ya TFRA yaleta mapinduzi shambani, Shilingi Bilioni 150 yaletaa majibu shambani

Ukurasa 12

## MAADHIMISHO MIAKA 24 BILA NYERERE...

# Rais Samia anavyotumikia maagizo ya kudumu ‘ujinga, umasikini, maradhi’ kwa mahitaji ya leo

**Na Peter Orwa**

KESHO ni kumbukumbu ya miaka 24 tangu kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere. Idadi hiyo ya miaka, inafafana na aliyotumikia urais wake, huku akiwa ameishi miaka 15 ya kustaafu.

Mwalimu Nyerere katika mfumo wa utumishi wake, alipenda sana kuunda kizazi cha uongozi, akiamini kingesaidia kutumiwa na taifa kurithi nafasi zao.

Alikuwa na sababu nyingi, ikiwamo uhalisia wa aliyokutana nayo wakati anarithi taifa kutoka mikono ya ukoloni. Hakuwa na viongozi wa kutosha kutumikia nchi, vilevile hata wataalamu wa stadi nyingine.

Hapo akapambana vya kutosha kusaka fursa za kuwaendeleza Watanzania ndani na nje ya nchi. Zao lake, akafanya ubunifu wa vyuo uongozi na vinginevyo nchini, kama cha TANU- Kivukoni Dar es Salaam na Chuo Cha Maendeleo ya Uongozi (IDM), Mzumbe, Morogoro.

Zao la waliojiunga na IDM baadaye, anapatikana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tena stadi yake akizama hasa aliko sasa, Utawala wa Umma (Public Administration), pasipo kujua mbele ya safari angekuwa mtawala hasa wa umma, ikizingtiwa kihistoria hajawahi kutoka nje ya mstari huo.

Leo, Dk. Samia anabeba dhamana ya Nyerere, nafasi ya urais wa nchi, akirejea pasipo kujua au huenda kutarajia zawadi na jukumu la kitaaluma alilopewa na mwasisi wa taifa kupitia aliochobuni- IDM, Morogoro.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa nchini India wiki hii. **PICHA: MTANDAO.**

Ni wiki hii akiwa nchini India alikotunukiwa shahada ya udaktari wa falsafa chuoni, vilevile kuingia mkataba ya kibiashara na uchumi na serikali ya huko, Rais Dk. Samia, anabaki katika kuendeleza historia ya namna hiyo kutoka uasisi wa nchi, maana, Rais Nyerere, amekuwa ‘damu damu’ na aliyekuwa Waziri Mkuu wake zama zile, Indira Gandhi.

Sura ya namna hiyo kimataifa, pia inaangukia katika juhudi binafsi za Dk. Samia katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) vyombo ambavyo Nyerere alivipenda sana.

Lakini, EAC ilingia dosari kabla ya kuanguka mwaka 1977 na kurejea kupishana na Nyerere kati kaumri wa mwisho, 1997 akiwa mstaafu.

Ndio katika picha ya pekee, China nayo rafiki wa kihistoria nchini, mwasisi akiwa Mwalimu Nyerere na rafikiye Mao Rais Tse Tung, nako zama hizi, Dk, Samia muda mfupi tu baada ya kupatia urais, akaenda huko kuimarisha uhusiano huo kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Hapo Katibu Mkuu wa chama chake, CCM, Daniel Chongolo, naye akaenda kunakishi uhusiano huo katika sura ya kichama, ambao nako wakongwe tangu zama za TANU walishajengea mizizi.

### MIRADI YA MAENDELEO

Ni baada tu ya kupata uhuru wa nchi, Rais Nyerere, akatangaza maadui wakubwa watatu kitaifa; ujinga, umasikini na maradhi. Mipango yake yote ililenga kukabili hayo na daima na haijawahi kubadilika hadi sasa.

Mipango ya maendeleo kuanzia wakati huo hadi sasa, haijawahi kutoka nje ya mstari wa kuwakabili maadui hao na kuwa sura pana ndio madhila makuu ya nchi zote masikini.

Inapoangaliwa kwa kina sasa, moja ya maeneo ambayo Mwalimu Nyerere alipenda sana kuweka nguvu zake ni kukabili ujinga, kwa kuwekeza nguvu ya kitaifa.

Ni katika elimu ilikuwa na hali ya ziada, ikipenya moja kwa moja katika sekta nyinginezo, Hapo Mwalimu Nyerere akaipa uzito, ikiwamo bajeti ya ziada kufika asilimia 25.

‘Kufumba na kufumbua’, miaka 13 baada ya uhuru, Tanzania ikawa katika orodha ya nchi duniani zinazofanya vizuri katika elimu ya msingi, hasa katika ‘kusoma na kuandika’ ambayo kwingi kuliwa katika hali mbaya.

Ni zama ambayo kundi kubwa lilibaguliwa hata kukosa fursa ya Kwenda shule. Baada ya uhuru wa nchi, serikali ilibeba dhamana ya wote waliokosa, ikiwamo kutokana fyursa finyu kwa mujibu wa mfuko wa kikoloni.

Uongozi wa Mwalimu Nyerere, ukawekeza elimu ikigusa sura kuu mbili. Mosi ni elimu ya msingi kufikia Watanzania wote, maana wakati huo kulikuwapo pengo kubwa na katika sura ya pili, elimu hiyo ilitolewa bure.

Leo hii katika zama za Dk. Samia, awamu tano baada ya Mwalimu Nyerere, siasa na uchumi ukiwa umehamia katika mfumo huria kutoka mfumo hodhi, kuna mambo kadhaa yanaendelezwa.

Serikali ya awamu ya sita katika kupigana kuendeleza maeneo ya kitaaluma kwa Watanzania wengi zaidi, bado inasimamia katika elimu ya bure msingi hadi kidato cha nne, iliyorejeshwa katika awamu iliyopita, Dk. Samia alipokuwa makamu wa rais.

Mfumo wa masomo na ada ulianza katika awamu ya pili, zama ambazo uchumi wa soko ulirejeshwa nchini, tangu kutoweka mwaka 1964, mwaka ambao Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ulianza, 1964 hadi 1969.

Inaendelea Uk 12

**UCHUMI**

SIKU YA MBOLEA DUNIANI…

# Nguvu ya TFRA yaleta mapinduzi shambani, Shilingi Bilioni 150 yaleta majibu shambani

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KILA ifikapo Oktoba 13 ya kila mwaka, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), inaungana na wadau wengine duniani kuadhimisha siku

hiyo muhimu kwa wanatasnia ya mbolea.

Siku hii kwa mara ya kwanza duniani iliadhimishwa 2016 nchini Uingereza, ambako maadhimisho ya siku hiyo ni mpango wa kimataifa

unaoungwa mkono na Jumuiya za Sekta ya Mbolea Duniani, ikiwa na lengo watu umuhimu na faida za mbolea, yakiwamo matumizi sahihi ya bidhaa hiyo, kwa mustakabali wa maendeleo endelevu.

Pia, Siku ya Mbolea Duniani, huadhimishwa kila mwaka tarehe hiyo ni kutokana na kumbukizi ya uvumbuzi wa kirutubisho aina ya 'amonia'

kinachopatikana hewani na uvumbuzi huo ulifanywa na mtafiti Fritz Haber mwaka 1908, ambaye ni raia wa Uingereza, ambao ulichochea mapinduzi ya kijani katika Karne ya 20.

Yanatajwa kuwezesha kuongezeka uzalishaji wa mazao kutokana na matumizi ya mbolea, yaliyosaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa njaa na

kuleta uhakika wa chakula katika nchi nyingi duniani.

**MADHIMISHO YALIVYO**

Maadhimisho ya siku ya Mbolea Duniani kwa mwaka huu, yanafanyika kwa siku tatu kuanzia Oktoba 11, 2023 hadi kilele chake, jana Oktoba 13,2023.

TFRA ikiwa mwandaaji na mratibu mkuu wa madhimisho hayo, yamefanyika katika Viwanja vya Chipukizi vilivyopo katika Manispaa ya Tabora Mjini, mkoani Tabora.

Maadhimisho hayo yameendana na maonyesho kutoka kwa wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo, hususani tasnia ya mbolea wakiwemo wazalishaji wa mbolea, kampuni zaidi ya 15

zilizoingiza na kusambaza mbolea nchini, pia mashirika na taasisi za kilimo na fedha.

Mafanikio yanayotajwa ni ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbolea 169, kuwatambua na kuongeza usajili wa wafanyabiashara kutoka 632 hadi 4,378, kuwafuatilia na kuwapa elimu ya utunzaji bora wa mbolea na utambuzi wa mbolea zisizokidhi viwango.

**MKURUGENZI WA TFRA**

Joel Laurent, Mkurugenzi Mtendaji ea TFRA, anasema ni hatua zilizozaa matunda ya kuongeza upatikanaji mbolea nchini, kutoka tani 429,814 kwa msimu wa mwaka 2016/2017 hadi tani 1,035,745 katika msimu wa 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 141.

Anasema, inafanya matumizi ya mbolea kuongezeka kutoka tani 296,036 mwaka 2016/17 hadi kufikia tani 580,529 msimu wa mwaka 2022/23, ambayo ni ongezeko la asilimia 96, ambalo ni baada ya serikali kupitia Wizara ya Kilimo, kuanzisha Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, ulioanza kutumika msimu wa kilimo 2017/2018.

Vilevile Joel anataja kuanzishwa Mpango wa Kutoa Ruzuku kwenye Mbolea zote za Kupandia na Kukuzia, katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali ilitenga shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kazi hiyo.



Shamba la mahindi lililopandwa na kukuzia kwa mbolea ya ruzuku msimu wa kilimo 2022/2023

Anasema katika maadhimisho hayo, wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za utafiti kampuni za mbolea, vyuo vikuu, mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau kilimo, watapata fursa ya kutoa elimu kwa wakulima.

Hiyo inajumuisha matumizi sahihi ya mbolea, pia kwa viuatilifu afya ya udongo, matumizi ya mbegu bora na udhibiti mbolea kwa ujumla.

Anasema lengo la Maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani, ni kupanua wigo zaidi wa kuelezea masuala mbalimbali katika tasnia ya mbolea ikiwemo mafanikio ya tasnia ya mbolea nchini, kutoa elimu kwa wadau wa mbolea hususani wakulima na wafanyabiashara wa mbolea.

Amefafanua kaulimbiu ya Siku ya Mbolea Duniani mwaka huu, "Ajenda 10/30 na Matumizi Sahihi ya Mbolea ya Ruzuku kwa Kilimo chenye Tija,"

Inaelezwa, serikali imetenga shilingi billioni 150 kwa ajili ya kutekeleza mpango wa utoaji wa Ruzuku kwa wakulima ili kuwapunguzia makali ya bei ya mbolea.

Kutokana na hilo anasema, kaulimbiu hiyo inalenga kuendana na jukumu kuu la TFRA; kusimamia ubora wa mbolea ili wakulima wapate mbolea bora na kisha kuongeza tija ya uzalishaji kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya chakula na malighafi za viwanda nchini na hata nje ya Tanzania.

Pia, anataja ukiwa mwendelezo wa kuwawezesha wakulima kupata mbolea kwa bei nafuu katika



Mfanyakazi wa kampuni ya mbolea, akifanya ukaguzi wa kitaalamu, kwa ajili ya kuwauzia wakulima. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**

mwaka wa fedha uliopo, 2023/2024 serikali imetenga shilingi bilioni 150 kwa ajili ya Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa wakulima wote nchini.

Joel anaeleza imani yake, kwamba mpango huo wa ruzuku, utaendelea kuchochea kuongezeka kwa matumizi ya mbolea na kukuza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kukifanya kilimo kuwa sekta inayochangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa.

Mkurugenzi huyo anafafanua, kwamba TFRA imefanikiwa kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja, akiainisha;tangu mwaka 2016/2017 hadi Septemba, 2023, jumla ya mbolea na visaidizi vya mbolea zilizosajiliwa zilikuwa 470.

Hiyo anataja ni ongezeko kwa mbolea zilizohakikiwa kufaa katika urutubishaji udongo, haya inayowawezesha wakulima kutumia mbolea zaidi, hasa kutokana na punguzo la bei kwao, litokanalo na ruzuku.

Kadhalika inatajwa uzalishaji mazao umeongezeka, katika msimu uliopita nchi imeweza kuzalisha mahindi zaidi, hata kudhibiti upungufu wa chakula nchini na mkulima kuongewa kipato.

Aidha, elimu ya matumizi sahihi ya mbolea imeendelea kutolewa na TFRA kwa kushirikiana na wadau katika sekta ya kilimo.

Mfumo huu umeboresha utoaji wa huduma kwa wateja ndani ya muda mfupi na kusaidia upatikanaji wa kumbukumbu za usajili wa wafanyabiashara wa mbolea na utoaji leseni,vibali vya kuingiza na kutoa mbolea nchini, pamoja na usajili wake.

Anasema, tangu mwaka 2016/2017 hadi Septemba, 2023, jumla ya mbolea na visaidizi vyake zilizosajiliwa zilikuwa 470, hivyo kuongezeka kwa mbolea zilizohakikiwa kufaa kwake katika urutubishaji wa udongo.

MKURUGENZI UDHIBITI MBOLEA

Happiness Mbelle, Mkurugenzi wa TFRA anayehusika na masuala ya udbhibiti, anasema serikali imetoa mafunzo kwa wakaguzi mbolea 169, kuwatambua na kuongeza usajili wa wafanyabiashara kutoka 632 hadi 4378, kuwafuatilia na kuwapa elimu juu ya utunzaji bora wa mbolea na utambuzi wa mbolea zisizokidhi viwango.

Mbelle anasema ongezeko hilo, ni baada ya serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuanzisha Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja ulioanza kutumika msimu wa kilimo 2017/2018,

Ni hatua inayowezesha wakulima kutumia mbolea Zaidi, kutokana na kupata punguzo la bei litokanalo na ruzuku, kadhalika uzalisha wa mazao umeongezeka

Aidha, anasema elimu ya matumizi sahihi ya mbolea imeendelea kutolewa na TFRA kwa kushirikiana na wadau katika sekta ya kilimo, kuoa na kuwapo mazingira mazuri ya biashara ya mbolea na Upatikanaji wa Mbolea za Ruzuku kwa mwaka 2022/23.

Mbelle anasema, wanaposherekea Siku ya Mbolea Duniani mwaka huu wameziona juhudi za Serikali katika kuimarisha tasnia ya mbolea na hususan kuweka mazingira wezeshi yanayovutia na kukuza uwekezaji katika tasnia ya mbolea na sekta ya kilimo kwa ujumla.

Mkulima, Yohana John, anasema msimu serikali imeanza mapema kuhimiza kilimo,ikiwemo matumizo sahihi ya mbolea,hivyo wakulima watafanya kilimo chenye tija ambacho kitawainua kuchumi.

## Rais Samia anavyotumikia maagizo ya kudumu 'ujinga, umasikini, maradhi' kwa mahitaji ya leo

Inatoka Uk 11

Kutokana kuwapo uwanda mpana wa kielimu, wastani wa vyuo vikuu zaidi ya 15 kutoka kimoja zama za Nyerere, elimu ya msingi imetapakaa kitaifa, sasa katika malengo ya taaluma, Rais Dk. Samia kaboresha, bila kuharibu tafsiri Nyerere, ikibaki palepale.

Ndani ya elimu bila malipo hadi kidato cha nne, umma unatajwa kuhamasika mno kupeleka watoto shule, huku mwendelezo wa serikali ya awamu ya sita ikifanya maboresho katika mitaala kukidhi mahitaji ya sasa.

Pia, kuna maboresho ya sheria zinazolenga elimu, ikiwamo katika ngazi ya sheria ndogo katika serikali za mtaa, ili kufanya elimu kuwa zao la manufaa kwa Watanzania kama ilivyokusudiwa na Mwalimu Nyerere, katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo, 1964 hadi 1969.

Katika ngazi ya vyuo, ili kutimza malengo ya Mwalimu Nyerere ya Mwaka 1964 kukabili ujinga kwa mahitaji ya leo, Dk. Samia anaamua kuwekeza kwea kuhakikisha wahitaji wote wa mkopo katika vyuo vikuu wanapatiwa tena bila ya riba.

Vilevile, hitaji hilo la kitaaluma, Rais Dk. Samia anawapa ofa maalum ya udhamini kundi la vijana kinamama wanaojiendeleza kitaaluma katika vyuo vikuu, huku shuleni kukiwapo mapitio ya mitaa kukidhi mahitaji ya leo, kama alivyofanya Mwalimu Nyerere, mwaka 1976.

Ndio mtazamo anaorejea nayn katika vita dhidi ya maradhi ambayo Nyerere akauweka katika Mpango wa Maendeleo wa 1964 - 1969 na kuendelea hadi anasatafu, huku Rais Jakaya Kikwete wa awamu ya tano akabuni Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), ambao una mazao ya kupendeza.

Rais Dk. Samia hapo 'anakabili maradhi' kwa kuanzisha mamia ya vituo vya afya, akiziba mapengo hata mikoa mpya isiyokuwa na hospitalil, inanufaika, ndai ya kipindi kifupi cha miaka miwili na nusu madarakani.

Kiuchumi, dhana ya Nyerere 'kilimo ni uti wa mgongo wa taifa' imetawala mipango yake, ukiwamo wa mwaka 1961 hadiu kustafau 1984

daima Dk. Samia hajakuwa nato mbao, mfano hai ukiwakatika miaka miwili ya fedha sasa, wizara hiyo imetengewa bajeti kubwa ya kihistoria nchini.

Ni bajeti inayoonyesha mageuzi makubwa katika sekta kilimo kukabili umasikini, shida ya ajira na njaa nchini, kukitarajiwa kuwekezwa katika kilimo cja kisasa cha umwagiliaji na cha kibiashara.

Watafiti kilimo kama TARI viyio vyua mbolea, uwekezaji mkubwa umeweka juu kiwango cha kilimo cha Tanzania, ngazi ya Afrika katika uzalishaji mbolea.

Hatua hizo za sekrikali awamu ya sita imeibua maboresho kwenye kilimo, kama kuwapo shamba la vijana kujifunza Bahi, Dodoma; Tanzania kuwa mwenyeji wa kilimo cha biashara Afrika, kilichoonyesha kwa mafanikio makubwa.

Mengine ni kupanuliwa wigo katika hifadhi ya nafaka kila mkoa, unaoendana na mfumo mpya wa kibiashara wa uuzaji mazao nje ya nchi na simu ya kisasa kuzalisja mpunga kibiashara Rufiji, huku kukitangazwa tani nyingi ya mazao kama ambazo kuuzwa kwa mafanikio nje ya nchi.

Sura hiyo inamuacha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kupita katika nyayo za Mwalimu Nyerere, kwa misingi ya mahitaji ya sasa.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Hili la urasimishaji ardhi jamani ugumu uko wapi?






**NA JOSEPH KULANGWA**

Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

WIKI iliyopita, nikiwa nimejituliza kama kasuku nikiangalia nchi hii inavyokwenda, nilimsikia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitoa maagizo ambayo kama kweli yatafanyiwa kazi, basi itakuwa afueni kubwa kwa baadhi ya Watanzania.

Nasema hivyo, kutokana na uzoefu niliyo nao kuhusu matamko ya viongozi wetu, ambayo mengi hupata fursa ya kusikika kwenye majukwaa ya kisiasa, huku sisi walalahoi tukishangilia, lakini turudipo majumbani na kuumwa njaa, ndipo hubaini tumepigwa.

Wanasiasa wa nchi hii wana talanta za kutumudu wawapo majukwaani, wakihimiza tuwapigie makofi, kana kwamba makofi si hisia za anayesikiliza, na ndiyo sababu mtu afiwapo hujikuta analia bila kuambiwa lia.

Hivyo, hata kupiga makofi mikutanoni hutokana na hisia, lakini wanasiasa wanapohutubia na kuona wasikilizaji mmechanganyikiwa, huomba makofi kama wasanii wanavyohimiza hadhira yao: "Mikono juu, mikono juu, piga makofi, piga makofi!"

Wanasiasa nao hutumia mbinu hiyo hiyo kutuvuruga, lakini nao kujidanganya kuwa tunawakubali na kuwaunga mkono, huku tukiwasujudia kuwa bila wao hakuna maisha duniani! Ni jambo la kushangaza sana, lakini ndiyo hali halisi ilivyo.

Waziri Mkuu alitoa maagizo kwa viongozi wa sekta ya ardhi kuchukua hatua dhidi ya kampuni zilizopewa majukumu ya kupima viwanja na kufanya urasimishaji, lakini zikashindwa kufanya hivyo kama inavyotakiwa.

Bahati mbaya sana, kumbe baadhi ya kampuni hizo zinamilikiwa na watendaji wa serikali ,wakiwamo viongozi wanaojifanya wajasiriamali wa kujipatia kipato kingine nje ya ajira zao, tena kwa kuwapa madeiwaka nyaraka za serikali.

Nyaraka hizo kwa mujibu wa Majaliwa, zinatumika kuuzia viwanja na hata nyumba, na kuikosesha serikali mapato. Hawa watu wapo na kumbe

wanajulikana, lakini ili wadhibitiwe, lazima Waziri Mkuu au Rais afanye ziara. Mambo ya ajabu kabisa haya! Waziri Mkuu Majaliwa anayajua matatizo yote haya, na ndiyo sababu amekuwa akizunguka huku na kule na kufukua madudu na kuchukua hatua sawia, ingawa uovu huu haukomi na unaendelea kwa njia mbalimbali.

Hebu fikiria tangu nchi hii ipate uhuru mwaka 1961 suala la upimaji ardhi limekuwapo likifanyika, lakini mpaka sasa kuna wajanja wanalitumia

kujinufaisha, hili la urasimishaji ardhi likaja enzi za Daktari JPM, ili angalau wananchi wenye vibanda au ardhi zao, wapate hati wakopee.

Hili nalo linakuwa gumu mpaka kuchukua miaka hedari na JPM alipotangulia mbele za haki, watu wakalipa kisogo na ndiyo sababu hata

watendaji wenyewe hawajui nini kilifanyika na kimefikia hatua gani mpaka sasa.

Kamishina Msaidizi wa Ardhi wa Jiji la Dar es Salaam… anasimama na kusema katika hilo la urasimishaji, watu wamelipa kati ya Sh 150,000 hadi Sh 250,000, hajui kuna watu walilipa Sh 300,000.

Hajui kuwa kuna watu wamewekewa bikoni tu kwa miaka yote hiyo na hawana hati kama yalivyokuwa matarajio na matamanio ya JPM, anaulizwa. anasema bila wasiwasi kwamba utakuta watu 1,000 wametambuliwa, lakini waliolipia ni 200 tu.

Anasema uchache wa waliolipia unakwamisha wengine, yaani anataka kutuambia, kwamba bila watu wote 1,000 kulipia, basi hata aliyelipia hatapewa hati yake. Sasa kulikuwa na maana gani kuomba mtu peke yake akalipie kiwanja chake benki. Kama utaratibu ungekuwa ni huo wa wote kulipa kwa pamoja, basiwangeachwa viongozi wa mitaa wachangishe mpaka zitimie, kana kwamba kipato cha kila mtanzania kinafanana! Huu ni ulaghai usio na msamaha kabisa.

Inashangaza hata Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na kukumbushwa kila mara naye alipitia njia hiyo hiyo ya 'mpaka wote walipe', kana kwamba ni nauli mpaka basi lijae!

Lakini cha kushangaza pia, ni kwanini serikali yenye wapimaji iruhusu kukodi kampuni binafsi kufanya kazi hizo, wakati wapimaji wakiendelea kulipwa mishahara yao kila mwezi, bila ya kufanya kazi walizoajiriwa!

Tulimsikia Waziri mwenye dhamana ya ardhi sasa, Jerry Silaa akitoa siku saba za kuchukuliwa hatua ya kuondoa mkwamo wa urasimishaji, ili waliotoa fedha zao wapewe hati na kama haiwezekani, warejeshwe walipie huduma zingine za kijamii.

Watanzania tumezoea kufanya kazi kwa nidhamu ya uoga na kujikomba, bila kubanwa mambo hayaendi na hasa pale viongozi wanapoona haya hayawahusu, kwani wana hati za mahekalu! Mungu atusimamie!

UCHUMI

## KINACHOJIRI WIKI YA VIJANA:

# Simulizi serikali inavyopigania vijana wake

**Na Agusta Njoji, Dodoma**

OKTOBA 8 hadi 14 kila mwaka, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana Ajira na Wenye Ulemavu huratibu Maadhimisho ya Wiki ya Taifa ya Vijana Kitaifa yenye lengo la kuwakutanisha vijana na kuwawezesha kubadilishana mawazo na kupeana maarifa ya kijamii na kiuchumi.

Katika maadhimisho haya shughuli zinazofanyika ni pamoja na maonesho ya shughuli za ubunifu na ujasiriamali kwa vijana pamoja na wadau mbalimbali wanaotoa huduma kwa ajili ya maendeleo ya vijana, midahalo itakayotoa fursa kwa vijana kujadili masuala muhimu ili kutatua changamoto zao,

Burudani na Michezo na shughuli za kujitolea. Pia huduma za ushauri nasaha, upimaji afya kwa hiari na uchangiaji wa damu salama zitafanyika.

Kwa mwaka 2023, maadhimisho haya yanafanyika katika Uwanja wa CCM stendi ya zamani Babati Mkoani Manyara yakiwa na kauli mbiu isemayo 'Vijana na Ujuzi Rafiki wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu'.

Mikopo kwa vijana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, anasema hadi mwaka 2023/24, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao upo chini ya Ofisi hiyo umetoa mikopo ya Sh.Bilioni 8.96 kwa miradi 1,126 yenye wanufaika 8,588.

Anasema hadi serikali inasimamisha utoaji mikopo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa lengo la kuboresha namna ya Utoaji mikopo, kiasi cha Sh. Bilioni 13.51 kilikuwa kimetolewa vikundi vya vijana 1,441.

Kukuza ujuzi Anasema Ofisi hiyo inatoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa nguvu kazi ya vijana iliyopo katika soko la ajira, yaani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo.

"Miongoni mwa programu za mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi zinazotekelezwa ni Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi ambayo inatoa aina za mafunzo ya kukuza ujuzi wa ufundi katika fani mbalimbali kwa njia ya Uanagenzi ambapo kijana anatumia zaidi ya asilimia 60 ya muda wa mafunzo katika maeneo ya kazi."



Vijana waliojiajiri wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO.**

Anasema tangu kuanza kwa mafunzo hayo mwaka 2016/17, vijana 133,448 wamenufaika kupitia programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi.

"Vijana 78,598 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na stadi mbalimbali za kazi kupitia mafunzo ya uanagenzi, 20,334 wamepatiwa mafunzo na kurasimishwa ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi wa mafunzo na kupatiwa vyeti ili wavitumie kutafuta ajira, kujiajiri na kujiendeleza kiujuzi katika taasisi mbalimbali za mafunzo,"anasema.

Anafafanua wahitimu 19,190 wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo wameunganishwa na fursa za mafunzo ya uzoefu wa kazi na kati yao 18,454 wamepatiwa mafunzo na taasisi za umma na binafsi ndani ya nchi na wahitimu 645 wameunganishwa na mafunzo ya uzoefu wa kazi nje ya nchi wakiwemo wahitimu 466 walioungan-ishwa kupata uzoefu wa kilimo cha kisasa nchini Israel.

"Vijana 13,088 wamepatiwa mafunzo ya kilimo cha kisasa ambapo kati yao vijana 12,580 ni wa mafunzo ya kilimo kupitia teknolojia ya kitalu nyumba, vijana 234 ni wa mafunzo ya kunenepesha mifugo, vijana 200 ni wa mafunzo ya ufugaji samaki na viumbe maji, na vijana 74 ni wa kilimo cha mazao kupitia vizimba,"anasema.

Anasema wafanyakazi 2,883 waliopo makazini (walioajiriwa na waliojiajiri) wamepatiwa mafunzo ya kuendeleza ujuzi wao katika fani mbalimbali ikiwamo za utalii na hoteli.

Utengaji maeneo Anasema hekari 274,047.50 zimetengwa kwa ajili ya shuguli za kilimo,ufugaji na shughuli nyingine za kiuchumi pamoja ma Mita za Mraba 540,642.50 zimetengwa katika maeneo ya kufanyia biashara kwenye halmashauri 176 na maeneo hayo hadi sasa vijana 193,053 wamenufaika.

Kadhalika, anasema kupitia programu ya Jenga Kesho iliyobora (BBT) kupitia sekta ya kilimo hadi sasa imeanzisha vituo vya mafunzo (Atamizi) 13 na vijana 812 wamenufaika na kugawiwa mashamba ambapo mwezi Oktoba 2023 wanatarajiwa kuanza uzalishaji.

Kuhusu mifugo na uvuvi, anasema vituo atamizi nane vyenye jumla ya vijana 238 wanawezeshwa kupitia programu ya unenepeshaji wa mifugo.

"Pia programu ya mafunzo atamizi ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa vijana kwa kushirikiana na sekta binafsi ambapo jumla ya vijana 200 wamepatiwa mafunzo haya na mpango wa serikali ni kuendelea kutoa mafunzo kwa vijana 750,"anasema.

PSSSF, NSSF, WCF na vijana Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma(PSSSF), CPA Hosea Kashimba, anasema mfuko umewekeza katika kujengwa kwa baadhi ya vyuo vya elimu ikiwamo Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Hombolo na Chuo cha Nelson Mandela ambapo uwekezaji huo umesaidia vijana wengi kupata elimu.

"Pia PSSSF kupitia ofisi zake mbalimbali nchini hupokea wanafunzi wengi wao wakiwa vijana kwa lengo la kupata mafunzo kwa vitendo .

Inabainishwa kuwa katika vyuo nane vya elimu ya juu na wanavyuo 1050 wameshajiunga na mpango wa kujichangia kwa hiari ambapo kwa sasa uhamasishaji na ufuatiliaji wa michango unaendelea.

Kuhusu uboreshaji wa fursa za ajira kwa vijana, anasema katika kutekeleza jukumu la uwekezaji NSSF inatengeneza fursa nyingi za ajira kwa vijana ili kuinua vipato vyao.

Vilevile, anasema katika kiwanda cha Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko (CPB), NSSF imeweza kuchangia katika eneo la ajira kwa vijana ambao hapo mwanzo walikuwa mtaani kutokana na kutoa mkopo wa Sh.Bilioni 3.6 kwa ajili ya kununua mashine ya kusaga unga pamoja na mafuta ya alizeti ili kuongeza thamani ya mazao hayo.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk.John Mduma anasema WCF ni taasisi ya Hifadhi ya jamii iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi [Sura 263] kwa lengo la kulipa fidia kwa wafanyakazi waliopo katika sekta ya umma na binafsi Tanzania Bara ambao wataumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi.

Anasema lengo la WCF ni kulinda nguvu kazi ya taifa kwa kuwa kijana ndiyo nguvu kazi ya taifa na mfuko unatoa mafao yanayomnufaisha moja kwa moja kijana hivyo kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuwekeza katika vijana walioko katika sekta mbalimbali.

Anasema WCF ni tofauti na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii kwani hutoa mafao kwa vijana bila kusubiri uzeeni na wafanyakazi hawachangii katika Mfuko huo wachangiaji ni waajiri peke yake.

Anabainisha kuwa kwa kuzingatia maslahi ya vijana na wategemezi wao WCF inatoa msaada wa mazishi na fao la kifo pale ambapo mtu atafariki kutokana na kazi.

"Wategemezi ambao ni wajane au wagane hulipwa pensheni kwa kipindi chote cha maisha yao na watoto hulipwa hadi wanapofikisha miaka 18 au zaidi iwapo wako masomoni,"anasema.

Anabainisha WCF inaongeza tija kwa kulinda ujuzi wa vijana nchini kwa kutoa fao la utengamao fao hilo linawezesha vijana kupata ujuzi mbadala endapo atapata ulemavu utakaozuia kufanya majukumu yake ya awali.

**OSHA INAYOWAGUSA VIJANA**

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, anasema taasisi hiyo ina wajibu wa kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vilivyopo katika sehemu za kazi ambavyo vinaweza kusababisha magonjwa na ajali na shughuli za OSHA zinawagusa vijana moja kwa moja.

"Vijana ni sehemu kubwa ya nguvukazi inayotegemewa katika shughuli mbali mbali za uzalishaji nchini. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni vijana takribani 800,000 huingia katika soko la ajira kila mwaka kati yao vijana wapatao 40,000 huingia katika ajira rasmi na wanaobakia huajiriwa au kujiajiri katika sekta isiyo rasmi,"anasema.





Kaimu Katibu wa Chama cha Wafugaji Kanda ya Kati (CCWT), Simon Ndaki, akizungumza na waandishi wa habari, wilayani Manyoni mkoani Singida juzi, kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili wafugaji katika eneo lake. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Uswisi yaridhishwa matokeo mradi wa afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI ya Uswisi imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa HPSS Tuimarishe Afya ambao umechangia mageuzi makubwa ya upatikanaji wa huduma za afya.

Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassoa, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha kuhitimisha mradi huo ambao umetekelezwa kwa miaka 12 kwa ushirikiano kati ya Uswisi na Tanzania katika kuimarisha mifumo ya afya.

Alisema mradi huo umekuwa na mafanikio makubwa ikiwamo mageuzi yaliyofanyika ya upatikanaji wa huduma za afya hasa vijijini ambako kwa muda mrefu upatikanaji wa huduma za afya ulikuwa duni.

Balozo Chassoa alisema wataendeleza ushirikiano uliopo katika sekta ya afya ili kufikia lengo la upatikanaji wa huduma za afya kwa wote kabla ya Mwaka 2030.

"Leo (jana) tunahitimisha mradi huu uliodumu kwa miaka 12 lakini bado tutaendelea kushirikiana katika maeneo mengine ili tufikie lengo la kila Mtanzania kufikiwa na huduma za afya. Mradi huu umekuwa na mafanikio makubwa kutokana na nia ya dhati ya serikali ya Tanzania katika kuboresha huduma za afya," alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, aliishukuru serikali ya Uswisi kwa ushirikiano wa muda mrefu na Tanzania katika sekta ya afya na kuahidi kuendeleza yote yaliyoanzishwa na mradi huo.

"Tunajivunia ushirikiano huu kwani unaendana na dhamira ya serikali ya awamu sita katika kufikia lengo la huduma ya afya kwa wote. Sera na ilani inayotuongoza ya chama chetu inatuagiza kuhakikisha kuwa hakuna tunayemuacha nyuma kwenye afya na tunatekeleza hilo kwa vitendo.

"Katika kufikia hilo tunapambana kuhakikisha kuwa kila mtanzania anakuwa na bima ya afya na nyinyi mmetusaidia hasa kwenye hii Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF)," alisema.

Awali, Meneja Mradi huo, Ally Kebby, alisema ulianza nchini mwaka 2011 katika mkoa wa Dodoma kwa lengo la kuimarisha na kuboresha mifumo ya afya nchini na hadi unakamilika umeifikia mikoa yote ya Tanzania Bara na umetekezwa na Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Alisema, kupitia mradi huo, wametimiza jukumu la kufanyia maboresho mfuko wa afya ya jamii kuwa bima ya afya na limefanikiwa kwa ushirikiano na wadau wengine na kwa sasa mfumo huo unatekelezwa na serikali yenyewe.

"Tulipewa jukumu la kuhakikisha tunakuja na ugunduzi mzuri wa afua zitakazosaidia kuboresha upotikanaji wa dawa na kuboresha menejimenti na matumizi ya dawa,tumefanya kazi hiyo pamoja na wizara mbili na tumetengeneza mifumo ya ugavi wa dawa,"alisema.

# MSD yawezesha vifaa tiba vya mil. 442/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BOHARI ya Dawa (MSD) kupitia Global Fund imetoa vifaa tiba na dawa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 442.3 katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida, Hospitali ya Wilaya ya Singida na Kituo cha Afya cha Itigi kwa ajili ya kuboresha huduma za matibabu.

Mhandisi wa vifaa tiba wa MSD Kanda ya Kati, Jumanne Mapesa, alikabidhi vifaa hivyo juzi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida ambavyo ni vitanda vya kisasa tisa vya chumba cha wagonjwa walio katika uangalizi maalum (ICU) na dawa vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 11.3.

Alisema kwa Hospitali ya Wilaya ya Singida vifaa vilivyotolewa ni vitanda viwili vyenye thamani ya Sh. milioni mbili wakati kwa cha Kituo cha Afya cha Itigi vifaa vyote vilivyotolewa vina thamani ya Sh. milioni 79.

Mapesa alisema utoaji wa vifaa hivyo ni mwendelezo wa uboreshaji wa huduma za sekta ya afya mkoani Singida kwa kuwa Machi 15, mwaka huu, MSD ilitoa vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Sh. nilioni 350 katika Hospitali ya Halmahsauri ya Wilaya ya Singida.

Alivitaja vifaa vilivyotolewa kuwa ni pamoja na mashine za kufulia, vifaa vya kinywa na meno, usingizi na vitanda .

Baada ya kukabidhi vifaa hivyo, wataalam kutoka MSD walitoa maelekezo kwa wataalam ambao hospitali zao zimenufaika na vifaa hivyo wavitunze ili vidumu muda mrefu kwa kuwa serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kuvinunua.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida, Dk. Paul Ndeki, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Singida, Yusuph Kitinya na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Itigi, Dk. Emmanuel Mallange, waliahidi kuvitunza na kuishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya nchini.

"Vifaa tulivyopatiwa vitatusaidia kutoa huduma katika hospitali zetu tunawashukuru Global Fund kwa ushirikiano mkubwa wanaoipa serikali na kufanikisha kupata msaada huu kupitia MSD hivyo kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi," alisema Dk. Kitinya.

Diwani wa Ilongero, Issa Mwiru, na mwenzake wa Itigi Mjini, Ally Minja, walipongeza serikali na MSD kwa msaada huo wa vifaa tiba na dawa kwani vitasaidia kuleta maboresho makubwa kwenye sekta ya afya mkoani hapa..

Mwiru aliishukuru Serikali kwa kuwaletea watumishi katika hospitali mpya ya Wilaya ya Singida na kusifia utendaji kazi wao kwa masaa yote wanapokuwa kazini.

# Wamiliki shule binafsi walia na utitiri kodi, tozo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAMILIKI wa shule zisizo za serikali wamewasilisha hoja na zaidi ya mapendekezo 10 kwa serikali ikiwamo kodi na utitiri wa tozo zinazoumiza uwekezaji binafsi kwenye sekta ya elimu.

Akisoma maazimio ya wamiliki hao katika kikao chao kilichoandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia juzi, Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wawekezaji Binafsi katika Elimu (TAPIE), Laurent Gama, aliomba upatikane mkakati wa kuangalia namna ya kupunguza au kuondoa kodi na utitiri wa tozo ili kulinda mitaji na uwekezaji kwenye sekta hiyo.

Kuhusu mitihani ya majaribio, alisema hakuna utaratibu mzuri wa upimaji, ujifunzaji na ufundishaji nchini hali inayosababisha utitiri wa mitihani inayoratibiwa na mamlaka mbalimbali za usimamizi wa elimu hasa ngazi ya kata, wilaya na mkoa.

"Bado hakuna mwongozo ulio wazi wa namna mitihani itakavyofanyika, wito wa kulipa fedha nyingi kwenye hii mitihani bado unaendelea kutolewa, tunashauri kuundwa kwa baraza la elimu jumuishi.

"Kuondolewa kwa kada ya walimu wa ngazi ya cheti katika mfumo wa ajira za wageni, tunashauri hawa walimu tuendelee kuwatumia hasa tunapoelekea kwenye elimu ya awali kuwa ya lazima kwa shule zinazofundisha kiingereza hali ni mbaya tukikosa walimu hawa," alisema.

Alisema kuna mwingiliano wa kiutendaji baina ya Wizara ya Elimu, sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI), hivyo kupendekeza kuundwa kwa chombo huru cha kuratibu na kusimamia elimu msingi nchini.

"Kuna mwingiliano wa majukumu wa wazi wa kimaslahi kabisa kati ya maofisa elimu wa mikoa na wilaya wakiwa wawakilishi wa Kamshina wa Elimupia wakiwa atumishi wa TAMISEMI. Kama mnavyofahamu maofisa elimu wa mikoa na wilaya wao wanamwakilisha kamishna kwenye maeneo yao lakini ni waajiriwa wa TAMISEMI," alisema.

Alisema nyadhifa hizo zinasababisha muingiliano kwenye majukumu yao na kushauri wapunguziwe majukumu.

Kadhalika, alisema kuna baadhi ya taasisi zinazosimamia elimu zimekuwa hazifanyi kazi kwa karibu na sekta binafsi.

Alisema jukumu la kuzisimamia na kuratibu taarifa hizo ni la TAMISEMI na kupendekeza takwimu zote zirudi mamlaka ya Wizara ya Elimu.

"Kumekuwa na kutonufaika kwa wazi kwa sekta binafsi na fedha zinazotolewa kama misaada, ruzuku au mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya elimu nchini zinazotolewa na wadau wa maendeleo, sisi kama wadau wa elimu tunahitaji pia kunufaika nazo,"alisema.





Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah (kulia) na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zambia, Lillian Bwalya wakibadilishana nyaraka, baada ya kutiliana saini makubaliano ya kutatua changamoto nane kati 24 za kibiashara kati ya nchi hizo, wakati wa mkutano wa pamoja wa kujadili changamoto hizo, uliofanyika katika Kituo cha Huduma za Pamoja Mpakani- Tunduma, mkoani Songwe juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Tanzania, Zambia zaanza utatuzi kero biashara mpakani Tunduma

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

TANZANIA na Zambia zimeanza mikakati ya kutatua kero 24 za kibiashara baina ya mataifa hayo mawili na mpaka sasa kero nane zimeshatatuliwa huku 16 zilizobaki zikitarajiwa kutatuliwa ifikapo Desemba, mwaka huu.

Miongoni mwa kero ambazo zimewekewa mikakati ya kutatuliwa ni kupunguza msongamano wa malori katika mpaka wa Tunduma mkoani Songwe ambao umekuwa ukisababisha baadhi ya bidhaa kuchelewa kufika sokoni.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, aliyasema hayo juzi alipozungumza na vyombo vya habari baada ya mkutano wa pamoja baina ya mataifa hayo uliolenga kujadili kero za kibiashara.

Mkutano huo ulifanyika katika kituo cha pamoja cha forodha cha Tundumba (One Stop Border Post) kuwashirikisha viongozi wa pande zote mbili.

Dk. Abdallah alisema nchi hizo zimekubaliana kuwa bidhaa zinazosafirishwa kutoka pande zote mbili kwenda nchi nyingine zikiwa na vibali vyote vinavyohitajika zinaruhusiwe kupitishwa bila kizuizi kulingana na makubaliano ya kibiashara ya Shirika la Biashara la Dunia (WTO) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Taasisi zote za umma zinazohusika na utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara baina ya nchi hizo zinatakiwa kuhakikisha hawawakwamishi, wanatakiwa kuwasaidia kutatua matatizo hasa upatikanaji wa vibali kulingana na Sheria," alisema Dk. Abdallah.

Alitoa rai kwa wafanyabiashara ya usafirishaji wa bidhaa mbalimbali kuhakikisha wanapata vibali vyote vinavyohusika kabla ya kuanza safari ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa hizo bila vikwazo na kuzifikisha katika nchi husika kwa wakati.

Vilevile, alisema serikali ya Tanzania imekubali kufanya mapitio na marekebisho ya tozo ya maendeleo ya reli kama inavyotekelezwa katika Itifaki ya Biashara ya SADC na kuharakisha mchakato wa kanuni za usafirishaji ili ziendane na kanuni za usafirishaji zinazotekelezwa katika Eneo Huru la Biashara la Utatu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Zambia, Lillian Bwalya, alisema nchi hiyo ilikubali kutatua kero hizo kwa pamoja ili kurahisisha na kukuza biashara za mpakani baina ya nchi hizo mbili.

Alisema baadhi ya makubaliano yaloyotiwa saini baina ya nchi hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji ikiwemo upanuzi wa barabara na kutekeleza mfumo wa upatikanaji wa vibali kabla ya kufika mpakani ili kuboresha mtiririko wa magari mpakani.

Alisema Zambia imekubali kutumia mfumo wa ufuatiliaji wa mizigo kwa njia ya elektroniki unaotekelezwa nchini Tanzania ama kuharakisha mchakato wa ununuzi wa mfumo unaopendekezwa kutumiwa na Mamlaka ya Mapato ya Zambia (ZRA).

Bwalya alisema, Zambia imekubali kuangalia uwezekano wa kutumia mfumo wa kisasa wa ufuatiliaji wa magari barabarani ili kuondoa na kupunguza vizuizi vya ukaguzi barabarani.

"Sisi Zambia tumekubali kutumia ofisi za jijini Dar es Salaam inayotolewa na serikali ya Tanzania kwa ajili ya Maafisa wa uondoshaji wa mizigo ya Zambia kuanza Desemba 31, 2023 ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kuondoa msongamano wa magari," alisema Bwalya.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha (Usimamizi na Uchumi), Elijah Mwandumbya alisema tozo na kodi mbalimbali zitaendelea kupitiwa na kurekwbishwa ili kuwezesha sekta binafsi kutumia fursa mbalimbali zinazojitokeza.

Balozi wa Tanzania nchini Zambia, Luteni Jenerali Mathew Mkingule, alisema kero zilizoondolewa zitaongeza ufanisi wa utoaji huduma na kukuza ushirikiano wa kibiashara baina ya nchi hizo.

# Njombe yageukia ujenzi shule shikizi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI, wadau wa maendeleo na taasisi mbalimbali mkoani Njombe wameombwa kuchangia ujenzi wa shule shikizi ya msingi katika eneo la Block X Kata ya Njombe Mjini ili kuwapunguzia watoto wa mtaa wa Kambarage adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta elimu.

Watoto wa eneo hilo wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita tano kwenda kusoma katika shule za msingi Mpechi na Kambarage, hivyo kusababisha wengi kuwa watoro

Ombi hilo lilitolewa na mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe, Erasto Mpete, alipotembelea eneo hilo la Block (X) ambalo litajengwa shule hiyo itakayokua na vyumba vya madarasa vitatu ofisi moja na matundu ya vyoo nane.

Mpete alisema alitembelea eneo hilo kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi wa mtaa huo kuhitaji kutatua changamoto iliyopo kwenye eneo hilo.

Alisema kwa jitihada za wananchi na ofisi ya mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe imetoa kibali cha ujenzi wa shule shikizi katika eneo hilo.

"Niwaombe wananchi,taasisi mbalimbali na wadau wa maendeleo kuweza kuchangia ujenzi wa shule hii ili kwa pamoja tuweze kupunguza changamoto kwa watoto wetu wanaotembea umbali mrefu.

"Tunaomba watu wetu walioteuliwa kuchangisha mchango wa ujenzi wakipita kuomba mchango wa kuchangia ujenzi huu tusisite kutoa,na ambaye anaweza kutoa chochote tunaomba atusaidie kama vile mchanga au mawe ili tukamilishe kwa wakati," alisema Mpete.

Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Mji Njombe, Shida Kiaramaba, alisema kutokana na uwapo wa ukatili kwa watoto mkoani Njombe, kuna haja ya kujenga shule hiyo ili kuwanusuru watoto wanaotembea umbali mrefu.

Ofisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Mji Njombe, Amos Luhamba, alisema eneo hilo lina ukubwa wa ekari 1.8 na shule utawasaidia wananchi wa mtaa huo kutatua changamoto na kuwalinda watoto wao.

"Nawaomba wananchi wa mtaa huu muhakikishe mnatunza mazingira kwa kupanda miti ambayo itasaidia kuongeza hewa safi," alisema Luhamba.

Mtendaji wa Kata ya Njombe Mjini, Enos Lupimo, alisema wamejipanga kuhakikisha ujenzi wa shule shikizi unaenda kwa kasi kubwa huku akisisitiza wananchi kuunga mkono ujenzi huo. Baadhi ya wazazi wa eneo la Block X akiwamo Solanus Mhagama, alisema watoto wao wanapata adha kubwa ya kupata elimu jambo linaloweza kudidimiza ndoto zao.

# CCM yataka miradi viporo kukamilishwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Deo Sanga, amewaagiza viongozi mkoani hapa kumalizia miradi yote viporo iliyoanzishwa na wananchi.

Alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha majumuisho ya kamati ya siasa mkoa akibainisha kwamba wamegundua kuwapo kwa changamoto katika sekta ya elimu hususani ujenzi wa maboma viporo ya madarasa na sekta ya afya.

"Vituo vya afya na zahanati havijakamilika, hivyo serikali kupitia halmashauri zote ikamilishe kwa haraka maboma hayo ili wananchi wapate huduma kiufasaha," alisema.

Sanga pia alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, kuunda tume ili kuchunguza miradi miwili ya mabwawa ya samaki Mtwango na kituo cha afya cha kijiji cha Ikondo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe ambayo haijakamilika huku fedha nyingi zikitumika.

Sanga alisema kamati ya siasa mkoa ilitembelea kata 81 kati ya 107 za mkoa na miradi 81 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 43 pamoja na mikutano ya hadhara na kusikiliza kero za wananchi.

Mtaka alisema kila halmashauri inatakiwa ijipange na kujua idadi ya miradi viporo ili kuikamilisha kwa wakati.

"Tujipange kwamba kwa mwaka wa fedha 2023/24 miradi hii inaenda kumalizika kwa sababu inawahusu wananchi ambao walichangia kwenye mapato yao. Waliuza mbuzi,kuku na vitu vingine," alisema.

Naye Katibu wa Siasa na Uenezi CCM Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga, aliwaonya baadhi ya viongozi wa chama hicho wanajihusisha na vitendo vya kukihujumu chama o kwa kuanza kuandaa wagombea wao watakaogombea nafasi mbalimbali ikiwamo udiwani na ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Luoga alisema chama hicho kimebaini uwapo wa viongozi wanaohujumu kazi zinazofanywa na wenyeviti,madiwani na wabunge waliopo madaraka kwa kuwasemea vibaya na kuwanadi watu wao na kuahidi kuwachukulia hatua kali za kinidhamu.





# 'Watoto wa kike wako kwenye hatari ya usalama wao'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATOTO wa kike Zanzibar wanakabiliwa na tatizo la usalama wao ikiwa ni pamoja na kubakwa na mimba za mapema, ambazo hukatiza ndoto zao za maisha na kudumaza ukuaji wao na maendeleo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas, katika maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike yaliyofanyika mjini hapa.

Alisema kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu, jumla ya matukio 1,081 ya ukatili na udhalilishaji yameripotiwa kwa mujibu wa mtakwimu mkuu wa Serikali, kati ya matukio hayo, 838 ni ya watoto wa kike na kupunguza nguvu kazi ya jamii katika ukuzaji wa shughuli za maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Alisema, utekelezaji wa fursa zinazohusu haki na ustawi na maendeleo ya mtoto zinatekelezwa kwa ufanisi, serikali inaendelea kuboresha huduma za malezi ya watoto wakiwamo wasichana kwa kutoa mafunzo ya malezi chanya kwa lengo la kuwezesha makuzi bora ya watoto.

Aliitaka jamii, taasisi za umma na binafsi kuendelea kusimamia na kushajiisha usimamizi wa ndoto za watoto wa kike ili zifikiwe kwa kuweka mikakati na fursa zitakazoinua vipaji, mipango na shughuli zao kufikia maendeleo endelevu.

Ofisa wa Ulinzi wa Mtoto kutoka Shirika la Save the Children, Mathias Busungu, alisema licha ya chagamoto zinazowakabili watoto, serikali inafavya kazi nzuri kuhakikisha mtoto wa kike anapata haki ya kuendelezwa.

Hata hivyo, aliitaka serikali kuongeza nafasi za ufadhili kwa ngazi za juu za elimu kwa watoto wa kike ili kutoa fursa na mwamko kwa watoto hao kusoma, kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Mtoto Zanzibar ya mwaka 2011 ili kutatua kero za watoto wa kike kulingana na mahitaji ya sasa.

Alisema ili kuendeleza vipawa vya uongozi kwa watoto, Save the Children wanaiomba serikali kuongeza bajeti ya uendeshaji wa mabaraza ya watoto kama ilivyo katika makundi mengine kwa kupendekeza angalau asilimia moja kati ya 10 ya makusanyo ya halmashauri ambayo inaelekezwa kwa wanawake, wazee na vijana ielekezwe pia katika uwezeshwaji wa mabaraza ya watoto.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Siti Abbas, alisema serikali inathamini mchango wa watoto na ndio maana kwenye sheria ya mtoto hakukuwa na ubaguzi.

Aliwataka watoto kuelewa moja ya majukumu yao ni kutojishughulisha na kitu chochote iipokuwa masomo.

Mwakilishi kutoka Shirika la Huduma ya Simu kwa Mtoto 'SISEMA' Masha Waziri, alisema watoto wa kike hawana mahali pa kutolea taarifa na kwamba namba 116 ipo rasmi kwa ajili ya watu kutoa taarifa zinazohusu udhalilishaji.



Sehemu ya wanafunzi 510 wa Shule ya Sekondari Mwawamiswe ya Kibaha, mkoani Pwani, wakifurahi baada ya kupokea msaada wa taulo 800 za kujisitiri kutoka kwa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (IMF) juzi, ikiwa ni mwendelezo wa mikakati ya taasisi hiyo kuwasaidia wanafunzi wa kike katika shule mbalimbali nchini kwa lengo la kuwafanya wasikose masomo wanapokuwa kwenye kipindi cha hedhi. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Wanaokwenda kuhiji waomba serikali kuwawezesha dola

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI zinazosafirisha mahujaji (UTAHIZA), zimeiomba Serikali ya Zanzibar kuingilia kati na kuwezesha mchakato wa upatikanaji wa fedha za kigeni kwa mahujaji ili kutekeleza ibada hiyo.

Mwenyekiti wa taasisi hizo, Ali Adam Ali, aliyasema hayo mjini hapa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kutokana na mabadiliko ya ratiba ya ibada ya hija.

Alisema kumejitokeza tatizo la uhaba wa dola, fedha inayotumika kwa ajili ya kufanya maandalizi ya safari za ibada ya Hijja na kuomba serikali kuingilia kati kufanikisha upatikanaji wa fedha hizo.

"Tunakabiliwa na tatizo la uhaba wa fedha za kigeni ambayo ni dola katika kufanikisha safari ya ibada ya Hijja nchini Mecca kwa hivyo tunaiomba serikali kuharakisha mchakato huo mapema," alisema.

Naye Katibu Mtendaji wa Wakfu na mali ya amana, Dk. Talib Abdalla Talib, alizitaka taasisi zinazosimamia mwenendo wa safari za ibada ya Hijja nchini Mecca kufanya maandalizi ya ibada hiyo mapema ikiwa ni maelekezo kutoka kwa Wizara ya Hijja na Umra ya Saud Arabia katika kufanikisha shughuli zote zinazofanyika huko.

Alisema katika miaka ya nyuma changamoto mbalimbali zilijitokeza na baadhi yake ilikuwa kikwazo katika utekelezaji wa ibada hiyo na kuibuwa malalamiko mengi kutoka kwa mahujaji.

"Wizara ya Hijja na Umra ya Saud Arabia imetutaka tufanye maandalizi ya safari mapema huku ikiweka ratiba ya utekelezaji wa mambo mbalimbali ya msingi kabla ya kufika Mecca," alisema.

Alisema wamepokea maagizo hayo kutoka kwa Wakfu ya mali ya amana ikiwa ni mwongozo unaowataka kufanya maandalizi ya mapema katika ibada hiyo pamoja na kuyazingatia masharti yote.

Alisema kwa zaidi ya miezi miwili, Benki Kuu ya Tanzania imethibitisha kuwapo haba wa dola kulikotokana na mwenendo wa hali ya uchumi duniani.

Aliyataja mambo ya msingi ambayo yanatakiwa kutekelezwa mapema kwa mujibu wa ratiba ni ifikapo Juni 30, 2023 ni mwanzo wa maandalizi ya Hijja kwa kila nchi kutangaza idadi kamili ya mahujaji.

Masharti mengine ambayo ni sehemu ya maandalizi ya mapema ni ifikapo Novemba 4, 2023, Mamlaka za Usafiri wa Anga nchini Saud Arabia inaanza kutoa vibali kwa nchi zitakazokuwa na ndege za moja kwa moja.

Aidha, Januari 8, 2024 ni mwisho wa vikao vya maandalizi ya Hijja na gharama zitakazotumika katika sehemu tofauti ikiwamo mahema na usafiri wa ndani.

Alisema kuanzia Machi mosi, mwakani viza kwa mahujaji wote duniani zitaanza kutolewa na Aprili 29, mchakato utafungwa.

Pia, Mei 9, 2024 mahujaji wote wenye nia ya kutekeleza ibada ya Hijja wataanza kuingia nchini Saud Arabia kwa ajili ya kutekeleza ibada ambayo ni miongoni mwa nguzo tano za dini ya kiislamu inayotakiwa kutekelezwa kwa kila Mwislamu mwenye uwezo.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetengewa nafasi ya kupeleka mahujaji 25,000 kila mwaka na mahujaji waliotekeleza ibada hiyo mwaka jana kutoka Tanzania ni 3,760 pekee.

# Mwinyi aishukuru Finland kuisaidia Zanzibar kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameishukuru Serikali ya Finland kwa jitihada za kuiunga mkono Zanzibar na kuisaidia kwenye masuala mbalimbali ya uchumi na maendeleo.

Dk. Mwinyi alitoa shukrani hizo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Balozi wa Finland nchini, Theresa Zitting.

Alisema hatua ya Serikali ya Finland ni kuisaidia Zanzibar kwenye sekta mbalimbali ikiwamo elimu, kilimo, afya, masuala ya wanawake hasa mapambano dhidi ya udhalilishaji wa jinsia kwa kushirikiana na taasisi na wanaharakati wanaopinga udhalilishaji wa wananwake na watoto.

Kuhusu sekta ya utalii, Rais Mwinyi alimweleza balozi huyo juhudi zinazochukuliwa na serikali yake kuiimarisha sekta hiyo inayochangia asilimia 30 ya pato la taifa.

Alisema, Zanzibar inaimarisha sera yake kuu ya uchumi wa buluu inayobeba mambo matano ikiwamo utalii, uvuvi, usafiri wa vyombo vya bahari, bandari, mafuta na gesi na kumueleza balozi huyo kuangalia fursa za uwekezaji kwenye maeneo hayo.

Alisema sekta ya utalii inajumuisha fukwe nzuri yenye mvuto kwa wageni pamoja na utalii wa urithi na kuongeza kuwa kuna fursa nyingi za uwekezaji na kuomba kuziangalia.

Akizungumzia sekta ya uvuvi, Rais Dk. Mwinyi alisema Zanzibar imejikita zaidi kwenye kilimo cha viumbe wa baharini ikiwamo ufugaji wa samaki na vifaranga, matango bahari na ukulima wa mwani ambao umenufaisha sehemu kubwa ya wanawake na vijana na kupunguza tatizo la ajira.

Kuhusu usafiri wa vyombo vya baharini Dk. Mwinyi alisema, unajumuisha bandari za Zanzibar, Dar es Salaam Pemba na Tanga kwa kusafirisha abiria na mizigo na kwamba kuna fursa nyingi za uwekezaji kwenye eneo hilo.

Pia, Rais Dk. Mwinyi alimuomba kuangalia ushirikiano wa kuiunga mkono Zanzibar kwenye miundombinu ya elimu, afya na nishati hasa kwenye masuala ya mifumo na vitendea kazi.

Naye, Balozi Theresa Zitting alisema Serikali ya Finland inafanyakazi kwa karibu zaidi na Serikali ya Zanzibar ambayo wanashikiriana kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo.

Alisema Finland imeshirikiana sana na Tanzania hasa kwenye sekta ya elimu, na kuimarisha miradi mingi ikiwamo uhifadhi wa mazingira, ardhi, misitu na masuala mengine ya maendeleo.

Balozi Zitting alisema Finland inathamini uhusiano na ushirikiano uliopo baina yao na Tanzania ikiwamo Zanzibar pamoja na nchi zote zilizopo Afrika Mashariki.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ROSELINE JOHN ONDITI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina la umiliki LAWI STEPHEN ODIERO yenye usajili namba T 724 CSC, CHASSIS NAMBA: KL1CD26RJ8B258348 na ENGINE NAMBA: 1224557K. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/24454/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MSELLA FESTOR CASTOR anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RAUM yenye usajili namba T 226 DKJ, CHASSIS NAMBA: NCZ200051125 na ENGINE NAMBA: 1NZB235330. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: PHQ/DOD/DOD/5112/2023

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 110 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late FIDELIS PETER ALCARD of Nzuguni within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SETH RWEKAZA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 01 Day of 11,2023

**Dated at Dodoma this 11 Day of 10, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 124 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late PAUL DAVIDI KIHOMBE**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY HARRY PAULO KIHOMBE**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of 10,2023

Dated at Dodoma this 04 Day of 10, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**
**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE SUB-REGISTRY OF MANYARA**
**AT BABATI**
**PROBATE AND ADMINISTRATION OF THE ESTATE CAUSE NO. 02 OF 2023**
**SIMONI GEHERI MANDO....................DECEASED**
**AND**
**SEVERA EVARIST KAROBAGWA.........PETITIONER**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18th Day of October,2023.

The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court. Dated at 15th Day of September,2023

**Deputy Registrar**
**Manyara**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH MAKORI MAGUCHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba **T 599 CXE,** CHASSIS NAMBA: **NCP610075524** na ENGINE NAMBA: **1NZB162276.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/4371/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH MAKORI MAGUCHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba **T 599 CXE,** CHASSIS NAMBA: **NCP610075524** na ENGINE NAMBA: **1NZB162276.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/4371/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

NAFTAL RASHID KIHWELO ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI MC 833CQB AINA YA TVS RANGI YA KIJANI.YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA PHQ/IRI/IRI/853/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MBUMI GIDEON MWAMBANDE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye usajili namba **T 890 CRF,** CHASSIS NAMBA: **ZCA260001223** na ENGINE NAMBA: **IZZ0548779.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/4372/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ALLY MPOMO LIWOWA anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 521 CXX TOYOTA NOAH. Chassis namba SR400265240. Engine namba 3S6059438. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: PHQ/MTW/MTW/785/2023.

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SARAH RAMADHANI MORADI** anatangaza kupotelewa na cheti cha Darasa la Saba chenye namba **PF17 0065875** kilichotolewa na ST. COLUMBUS PRIMARY SCHOOL mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/25114/2023.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Mabomu yaliyotupwa na ndege yakiharibu mji wa Gaza na kusababisha watu kuishi kwa hofu. **PICHA: REUTERS**

# ISRAEL YAITIFUA GAZA

## •Hakuna kinachoingia wala kutoka
## •Mabomu yachimbua ardhi,majengo

ISRAEL imetangaza itaendelea kuuweka ukanda wa Gaza katika mzingiro ambao hautaruhusu kitu chochote kuingia wala kutoka mpaka raia wake waachiliwe huru.

Waziri wa Nishati wa Israel, Israel Katz alisema wanajeshi wa nchi yake hawataacha kuishambulia hadi mateka wao watakapoachiwa huru bila masharti.

Katika chapisho la mitandao ya kijamii Katz, alisema hakuna swichi ya umeme itakayowashwa, hakuna bomba la maji litakalofunguliwa na hakuna lori la mafuta litakaloingia eneo hilo.

Israel ilisimamisha usambazaji wa bidhaa kwa Ukanda wa Gaza baada ya mashambulizi ya Hamas yaliyofanyika Jumamosi iliyopita.

**HALI MBAYA**

Imeelezwa hali ya maisha ndani ya gaza ni mbaya baada ya siku tano za mashambulizi ya mabomu.

Nishati ya umeme imekatika kuanzia jana baada ya kituo pekee cha kuzalisha umeme katika eneo hilo kukosa mafuta. Ilielezwa hospitali zimeelemewa baada ya kujaa maelfu ya majeruhi ambao wamekosa huduma ya matibabu.

Umoja wa Mataifa ulisema watu nusu milioni wa Gaza hawajapata mgao wao wa chakula tangu Jumamosi.

Umetoa wito wa kuanzishwa eneo la kibinadamu. Afisa mmoja wa Misri aliiambia BBC kwamba serikali mjini Cairo ilikuwa katika majadiliano na pande zote kujaribu kuruhusu msaada kuingia Gaza kupitia Misri hata kama ni kwa saa chache.

Wakati huo huo, kuna matarajio makubwa kwamba Israel hivi karibuni itaifanya mashambulizi ya ardhini.

Msemaji wa Israel alisema vikosi vinavyojumuisha askari wa akiba 300,000, walikuwa karibu na mpaka wakijitayarisha kwa kwa mashambulizi.

Jeshi la Israel pia limeimarisha kwa kuweka ulinzi mkali eneo lake la kaskazini na maelfu ya wanajeshi wanakabiliana na mashambulizi ya makombora kutoka Lebanon.

Katika taarifa yake ilisema jeshi lilishambulia maeneo ya wapiganaji nchini Lebanon baada ya makombora mawili kutua katika kituo cha kijeshi cha Israel karibu na mpaka

Watu watatu walijeruhiwa katika shambulizi hilo lililopiga miji na vijiji kadhaa, vyombo vya habari vya serikali ya Lebanon vilisema.

Hezbollah ilisema kuwa makombora hayo lilikuwa ni jibu la mauaji ya wapiganaji wake watatu yaliyofanyika Jumatatu.

Kikosi cha Ulinzi cha Israel (IDF) kilisema kombora lilorushwa kutoka kwenye kifaru cha Lebanon lilipiga kituo cha kijeshi cha Israel karibu na kijiji cha Arab al-Aramshe, ambacho kiko kusini mwa Mji wa Blue Line uliotengwa na Umoja wa Mataifa kutenganisha Israel na Lebanon.

Hezbollah ilisema ilifanya mashambulio hayo katika kulipiza kisasi kwa uchokozi wa Israel.

Ilidai kuwa kombora hilo lilisababisha majeruhi kadhaa ndani ya Israel.

**NDEGE KUITIFUA GAZA**

Jeshi la Israel lilisema mashambulio yake ya anga katika ukanda wa Gaza yanalenga kuharibu vichuguu ambavyo kwa miongo kadhaa vimetumika kama vituo vya operesheni kutoka kwa Hamas.

"Fikiria ukanda wa Gaza kama safu moja ya raia na safu nyingine ya Hamas," Jonathan Conricus, msemaji wa Jeshi la Ulinzi la Israel alisema katika ujumbe wa video uliotumwa kwenye mtandao wa X.

Alisema, njia hizo za chini kwa chini zilizojengwa kwa miaka mingi tangu Hamas kuchukua mamlaka mjini Gaza mwaka 2007, zimetumika kama njia ya kuhamisha vifaa na pia kupanga na kuanzisha mashambulizi dhidi ya Israel,.

Ukubwa na umuhimu wa njia hizo umefichwa na nyumba za watu juu ya ardhi ambazo nyingi sasa zimekuwa magofu.

"Kuna mengi zaidi ya inavyoonekana. Jeshi la anga la Israel limekuwa likishambulia vitongoji vingi vya Gaza. Kipaumbele chetu kwa sasa ni kuwalenga makamanda wanaofanya mashambulizi, na viongozi wakuu wa Hamas katika ngazi zote," alisema.

**WANAVYOSEMA VIONGOZI**

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz ameliambia bunge jana asubuhi kuwa yeyote anayeiunga mkono Hamas, au kuchoma bendera za Israel atakabiliwa na mashtaka ya jinai.

Alisema kundi linalounga mkono Palestina liitwalo Samidoun litapigwa marufuku.

Aliwashutumu wanachama wake kwa kuingia katika mitaa ya eneo la Neukölln mjini Berlin siku ya Jumamosi kusherehekea mauaji ya raia wa Israel kwa kuwagawia pipi wapita njia.

"Hii ni mbaya, huu ni unyama. Hatukubalia chuki na uchochezi. Hatutavumilia chuki dhidi ya Wayahudi." Aliliambia Bunge

Scholz pia alitangaza kupiga marufuku shughuli zote za Hamas nchini Ujerumani.

Kundi hilo tayari limetambuliwa kama kundi la kigaidi katika Umoja wa Ulaya, Uingereza na Marekani.

Huku Israel ikiendelea kushambulia ngome za Hamas mjini Gaza, rais wa Iran ameishutumu Israel kwa kufanya "mauaji ya halaiki"..

Nchi ya Iran ambayo inajulikana kufadhili na kuiwezesha Hamas kuendesha harakati zake Gaza imepongeza mmashambulizi hayo.

Kiongozi Mkuu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei alisema nchi yake haiko nyuma ya mashambulizi mabaya yaliyofanywa na Hamas.

**BLINKEN ATUA**

Waziri wa mambo ya nje wa Marekani Antony Blinken aliwasili jana nchini Israel.

Katika ziara yake hiyo fupi, Blinken alikutana na viongozi wa Israel na Rais wa Palestina Mahmoud Abbas.

## Shule zapatiwa madawati kukabili uhaba wa samani

**Na Mwandishi Wetu, KIBAHA**

RIPOTI ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Aprili 2017, ilibainisha uhaba mkubwa wa miundombinu na samani katika shule zinazomilikiwa na serikali.

Katika kukabiliana na uhaba wa samani shuleni na kuimarisha mazingira ya utoaji elimu nchini, Benki ya NMB imetoa msaada wa madawati, viti na meza kwa shule tano za msingi wilayani Kibaha mkoani Pwani vyenye thamani ya Sh. milioni 25.

Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper amekabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson Simon, aliyepokea kwa niaba ya Wakuu wa Shule za Kambarage, Lumumba, Kongowe, Bungo na Viziwaziwa, hafla iliyofanyika viwanja vya Shule ya Kambarage.

Katika makabidhiano hayo, Prosper alisema utatuzi wa changamoto za elimu Tanzania ni miongoni mwa vipaumbele vya benki hiyo kwa kuwa inaamini elimu ndio ufunguo wa maendeleo ya taifa lolote duniani.

"Tunatambua jitihada za dhati na za makusudi zinazofanywa na serikali katika kuboresha miundombinu na mazingira ya elimu mijini na vijijini, ndio maana hatuna budi kuipongeza na kuiunga mkono.

"Pamoja na makubwa yanayofanywa na serikali, sisi kama wadau vinara wa maendeleo tunao wajibu wa kuisapoti kustawisha jamii yetu, ambayo imeifanya NMB kuwa hapa ilipo – ikiwa ni benki kubwa na bora zaidi Tanzania, yenye mtandao mpana unaojumuisha matawi 230.

"Mheshimiwa mgeni rasmi, leo tunakabidhi msaada kwa ajili ya shule tano unaojumuisha madawati 200 kwa ajili ya wanafunzi wa Shule za Msingi Kambarage, Lumumba, Bungo na Kongowe - zinazopata madawati 50 kila moja, huku Viziwaziwa ikipata viti 16 na meza nane za walimu.

"Ni vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 25, ambayo ni sehemu ya Sh. bilioni 6.2 tulizotenga kwa ajili ya Programu ya Uwekezaji kwa Jamii (CSI), ambayo imekuwa na utaratibu endelevu wa kutoa asilimia moja ya faida yake kwa jamii, tukifanya hivyo kwa miaka saba mfululizo," alisema.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya Nickson aliishukuru NMB kwa msaada huo unaokwenda kuwatoa sakafuni wanafunzi 600, huku akibainisha kuwa serikali pekee haiwezi kumaliza kwa haraka na wepesi changamoto zinazokwaza sekta hiyo, hivyo inahitaji nguvu za wadau.

"Mnachokifanya mnaunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amefanya makubwa katika elimu Tanzania, na hapa Kibaha pekee kwa mfano mwaka huu ametuwezesha kujenga sekondari mpya mbili, shule za msingi mpya mbili na tumeajiri walimu wapya 900.

"Tumesikia changamoto ya madawati hapa Kambarage kama yalivyoainishwa na Mwalimu Mkuu (Happiness Msaki), ina maana yaliyotolewa na NMB yamevuka nusu ya uliokuwa upungufu. Tungetarajia kuona mdau akitoa asilimia 20 au 25, lakini NMB imetoa zaidi ya asilimia 50," alisema.

# TANZANITE HESABU KALI IKIWAKARIBISHA NIGERIA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwaondoa Djibouti, Kocha Msaidizi wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), Esther Chabruma amesema kikosi chake kina kazi kubwa kuelekea mechi inayofuata watakayocheza dhidi ya Nigeria.

Tanzanite imesonga mbele katika mashindano ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia (U-20), baada ya kuifunga Djibouti jumla ya mabao 12, ikishinda magoli 5-0 katika mechi ya kwanza na juzi ikawachapa wapinzani hao mabao 7-0, michezo yote ilichezwa kwenye Uwanja wa Azam, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kuwaondoa Djibouti, Chabruma alisema mechi haikuwa rahisi kwa sababu wapinzani wao walibadilika tofauti na walivyokuwa katika mchezo wa kwanza.

Chabruma alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kuzingatia maelekezo waliyowapatia kwenye uwanja wa mazoezi na kuyafanyia kazi vyema na hatimaye kupata ushindi wa mabao 7-0.

"Tulitoa maelekezo tofauti kwa wachezaji kuhusu mechi ya leo (jana), baada ya kuona mapungufu ya mchezo wa kwanza, nashukuru walizingatia hadi tukafunga mabao mengi, tunasahau matokeo hayo na tunarudi uwanja wa mazoezi kujiandaa na mchezo mwingine dhidi ya Nigeria.

Hakuna mechi rahisi Nigeria, ni timu ngumu ukizingatia tuliwahi kukutana nao katika michuano ya Kombe la Dunia U-17, Tanzania tuliondolewa hatua ya robo na wao walifika nusu fainali," alisema Chabruma.

Alisisitiza hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ya ubora wa Nigeria na hawana muda wa kupoteza kwa sababu wanahitaji kuwavaa wakiwa imara na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Mwisho wa mchezo huu ni mwanzo wa maandalizi ya mchezo huo ujao, tutajipanga ili kuhakikisha tunafanikiwa kuipeleka Tanzania katika fainali za Kombe la Dunia kwa mara nyingine," Chabruma alisema.

# KMKM, Malindi mechi ya kibabe

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKONGWE Malindi SC wanatarajia kuvaana na mabingwa watetezi, KMKM katika mechi ya mzunguko wa sita wa Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mao.

Malindi inashuka uwanjani ikiwa katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kujikusanyia pointi nane wakati KMKM yenyewe ikiwa ya tatu na alama zake 10 mkononi, timu hizo zilifungwa mechi zao zilizopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Malindi, Sheha Khamis alisema wamejipangaa kushuka dimbani kupambana na timu ambayo ni ngumu.

Khamis alisema anafahamu wapinzani wao ni wazoefu wa mashindano mbalimbali lakini pia wanataka kuhakikisha wanatetea taji la ubingwa wanalolishikilia.

Aliongeza Malindi imejipanga kucheza soka safi na wamewataka wachezaji wao kutokuwa na papara ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

"Tunaenda kucheza na timu yenye wachezaji wazoefu katika Ligi Kuu Zanzibar, simaanishi kama sisi hatuna wachezaji wazoefu hapana, lakini mchezo wenyewe jinsi utakavyokuwa uwanjani ni mgumu kwa timu zote, nimezungumza na wachezaji tunashuka uwanjani kwa kusaka alama tatu hivyo wasiwe na hofu ya mchezo mapema," alisema Khamis.

Kocha huyo aliongeza malengo ya timu yake msimu huu ni kuhakikisha wanamaliza katika nafasi nne za juu, hivyo watanarajia kucheza katika kiwango bora.

Bingwa wa ligi hiyo hupata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayofanyika kila mwaka na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

## Mashujaa yasikitika kuwakosa Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

NYOTA wa Mashujaa FC wamesikitishwa kuona mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba iliyotarajiwa kuchezwa Oktoba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika imeondolewa katika ratiba na kudai waliihitaji sana kwa ajili ya kujitangaza.

Akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, nahodha wa timu hiyo, Said Makapu alisema walikuwa wamejiandaa vyema na mechi hiyo ambayo walifahamu ingeshuhudiwa na mashabiki wengi huku wao wakitaka kuonyesha ubora wao.

Makapu, ambaye aliwahi kuichezea Yanga, alisema kila mchezaji alikuwa anajua ndiyo siku yao ya kujiweka sokoni, lakini baada ya kuahirishwa wamenyong'onyea ingawa wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuivaa Coastal Union.

"Tunajua Simba ni timu kubwa, tunawaheshimu lakini tulikuwa tayari kuwavaa, kila mtu alihitaji kuonyesha uwezo wake, sisi kama wachezaji tulikuwa tunaitamani sana hiyo mechi kwa sababu kila mmoja alitaka kuonyesha ana uwezo kiasi gani ili kumrahisishia kwenye soko,"

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

# TAARIFA YA MKUTANO MAALUM

## TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

TAARIFA INATOLEWA kwamba Mkutano Maalum **("Mkutano Maalum")** wa wanahisa **("Wanahisa au Wanachama")** wa Tanga Cement PLC utafanyika saa 4.00 asubuhi tarehe 10 Novemba 2023 kwa njia ya mtandao kupitia jukwaa la Microsoft Teams *https://bit.ly/3t0FBlw* (kwa kupitia kiungo kitakachotumwa kwa barua pepe na ujumbe mfupi wa simu kwa wanahisa, Pamoja na kiungo kilichooneshwa kwenye ukurasa wa jalada) na, kwa wale wanaochagua kuhudhuria ana kwa ana, Ukumbi wa Marquee, Serena Hotel, Dar es Salaam, kwa madhumuni ya kuzingatia na, ikiwa itaonekana inafaa, kupitisha (kwa au bila marekebisho) maazimio yaliyowekwa hapa chini.

Tarehe ya kumbukumbu ambayo Wanahisa wanapaswa kurekodiwa kama ilivyo katika rejesta ya wanahisa ya Tanga Cement kwa madhumuni ya kuamua ni Wanahisa gani wanastahili kuhudhuria na kupiga kura katika Mkutano Maalum ni Jumatatu tarehe 6 Novemba 2023.

**AZIMIO MAALUM NAMBA 1**

**KUTHIBITISHWA KWA MAPENDEKEZO YA UUZWAJI WA HISA 43,504,403 ZA KAWAIDA ZA TANGA CEMENT NA MNUNUZI KUTOKA KWA MUUZAJI KWENDA KWA MNUNUZI**

"ILIAMULIWA KWAMBA: Ununuzi Unaopendekezwa, ukiwa ni ununuzi kama inavyokusudiea katika Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Ununuzi Uliokusudiwa Uchukuaji na Uunganishaji) Kanuni za mwaka 2006 (Kanuni) na Kanuni za PLC za Soko la Hisa la Dar es Salaa, za mwaka 2022, ziidhinishwe na hivyo kupitishwa kuwa azimio maalum."

**AZIMIO MAALUM NAMBA 2**

**UTEUZI WA WAKURUGENZI**

"IMEAMULIWA KWAMBA, kulingana na ununuzi unaopendekezwa kutekelezwa kuanzaia tarehe ya utekelezaji huo:

2.1 uteuzi wa Bw Hakan Gurdal kama mkurugenzi wa Tanga Cement kuwa hivyo na kuthibitishwa na azimio maalum;

2.2 uteuzi wa Bw Dominik Michel kama mkurugenzi wa Tanga Cement kuwa hivyo na kuthibitishwa na azimio maalum;

2.3 uteuzi wa Bw Francesco Brambilla kama mkurugenzi wa Tanga Cement kuwa hivyo na kuthibitishwa na azimio maalum."

**AZIMIO MAALUM NAMBA 3**

"ÏMEAMULIWA KWAMBA: Wakurugenzi wawili wa Tanga Cement watakuwa wameidhinishwa kufanya mambo yote, kusaini nyaraka zote na kuchukua hatua kama inavyotakiwa (Pamoja na, lakini bila ya ukomo katika utekelezaji wa mikataba na nyaraka zote kama inavyotakiwa) na kwa ujumla kufanya lolote muhimu, au kuhitajika kutekeleza na kutekeleza maazimio haya na hatua zote kama hizo zilizochukuliwa kabla ya hapo zitaidhinishwa"

**MAPENDEKEZO YA WAKURUGENZI**

Kila mkurugenzi anapendekeza kuwa Wanahisa wapige kura kuunga mkono kila azimio

Kwa Agizo la Bodi

**Quresh Ganijee**
Katibu wa Kampuni

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

# TAARIFA KWA WANAHISA

## TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa ishirini na nane wa wanahisa wa Tanga Cement PLC utafanyika katika Ukumbi wa Marquee, Serena Hotel, Dar es Salaam na kwa njia ya mtandao wa mawasiliano wa kidigitali wa Microsoft Teams kupitia kiungo: bit.ly/46kFU96, siku ya Ijumaa tarehe 10 Novemba 2023 kuanzia saa tatu (3:00) kamili asubuhi kwa madhumuni yafuatayo:

1. **Taarifa ya Mkutano**
   Taarifa ya kuitisha mkutano ichukuliwe kama inavyosomeka.
2. **Kuidhinisha Kumbukumbu**
   Kuidhinisha na kusaini kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa ishirini na saba uliofanyika tarehe 25 Februari 2022
3. **Taarifa za Fedha na Ripoti za Wakurugenzi**
   Kupitia na kupitisha Taarifa za Fedha na ripoti za Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2021 na 31 Disemba 2022
4. **Gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2021 na 31 Disemba 2022**
   Wanahisa kuzingatia pendekezo kutoka Bodi la kutotangaza gawio la miwsho kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 31 Disemba 2021 na 31 Disemba 2022.
5. **Marekebisho ya Memoranda na Vifungu vya Kanuni za Makampuni**
   Kuthibitisha marekebisho kwenye Memoranda na Vifungu vya Kanuni za Makampuni
6. **Uthibitisho na Uteuzi wa Wakurugenzi**
   Kuthibitisha na Kuteua Wakurugenzi wa Bodi.
7. **Kuidhinisha Mapato ya Wakurugenzi**
   Kuidhinisha mapato ya Wakurugenzi kwa mwaka wa fedha 2023.
8. **Uteuzi wa Wakaguzi wa Nje**
   uidhinisha uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa mwaka wa fedha 2023.
9. **Majumuisho**
   Mengineyo.

Mwanachama yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano ana haki ya kuchagua mwakilishi au wawakilishi na kupiga kura kwa niaba yake. Endapo mwanachama ni shirika basi mwakilishi anatakiwa fomu za uwakilishi pamoja na maamuzi ya Bodi ya kumteua mwakilishi huyo. Fomu hizo zifike katika ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni si chini ya masaa 48 kabla ya muda wa mkutano kuanza. Wanachama na wawakilishi wanatakiwa kuja na risiti ya amana na uthibitisho wa kupokea fomu ya uwakilishi, nakala ya fomu za uwakilishi na ukitambulisho kwaajili ya usajili.

**Kwa agizo la Bodi.**

Quresh Ganijee
**Katibu wa Kampuni**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**JORGINHO KUTUA BARCA**
BARCELONA inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 31. **(Mirror)**

**LINGARD ANUKIA SAUDIA**
JESSE Lingard ameongeza nafasi yake ya kuhamia klabu ya Al-Ettifaq ya Saudi Arabia baada ya kuifungia timu ya Steven Gerrard katika mechi ya kirafiki iliyochezwa juzi. Mshambuliaji huyo wa England amekuwa hana timu tangu alipoondoka Nottingham Forest msimu huu wa joto. **(Goal)**

**OSIMHEN ATAJWA CHELSEA**
CHELSEA imemwongeza mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24 kwenye orodha ya walengwa wa uhamisho wa dirisha la Januari. **(ESPN)**

**ALONSO YUKO HURU**
BOSI wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso mwenye umri wa miaka 41, ana kipengele katika mkataba wake ambacho kitamruhusu kuwa kocha klabu zake zote za zamani - Liverpool, Real Madrid au Bayern Munich - mapema msimu ujao wa joto. **(Bild, Via Mail)**

**GUIRASSY AGOMBEWA EPL**
KLABU za West Ham, Brighton, Crystal Palace na Bournemouth zinavutiwa na mshambuliaji wa Stuttgart na Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 27, ambaye ndiye mfungaji bora wa Ligi Kuu Ujerumani (Bundesliga) kwa sasa msimu huu. **(90min)**

**WAN-BISSAKA MAMBO SAFI**
KLABU ya Manchester United inatazamiwa kuongeza mkataba wa beki wa pembeni wa England, Aaron Wan-Bissaka (25) na mlinzi wa kati wa Sweden, Victor Lindelof (29), lakini itachukua muda wao kabla ya kuamua mustakabali wa fowadi wa Ufaransa, Anthony Martial (27). **(ESPN)**

**CONTE AIKATAA NAPOLI**
KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte amekataa nafasi ya kuwa kocha ajaye wa Napoli, huku Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 54 akipendelea kusubiri nafasi kwingine. **(Fabrizio Romano)**

**HOJBJERG ANUKIA JUVE**
JUVENTUS inataka kumsajili kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28 ifikapo Januari. **(Gazzetta dello Sport)**

**SOUCEK ATAKIWA INTER**
KLABU ya Inter Milan inalenga kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Czech, Tomas Soucek mwenye umri wa miaka 28. **(Calciomercato)**

**TIELEMANS NJIA MOJA**
KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 26 anataka kuondoka Aston Villa baada ya kutofautiana na Kocha, Unai Emery. **(Football Insider)**

**BARCA YAMTAKA VARELA**
BARCELONA inamfuatilia kiungo wa kati wa FC Porto, Alan Varela mwenye umri wa miaka 22. **(Mundo Deportivo)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED HAIJAAMUA HATIMA YA MARTIAL

●●● Mabosi wa klabu hiyo waweka wazi bado wana muda wa...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United iko tayari kuongeza mkataba wa Aaron Wan-Bissaka na Victor Lindelof, vyanzo vimeiambia ESPN, lakini mabosi wa klabu hiyo wamejipa muda kabla ya kufanya uamuzi juu ya hatima ya Anthony Martial.

Mfaransa huyo, ambaye ana mkataba hadi mwisho wa msimu pamoja na chaguo la kuongeza mwaka mmoja, alikumbwa na majeruhi msimu uliopita ambapo alianza mechi 11 pekee za Ligi Kuu England.

Kwa sasa amepoteza namba kwa mchezaji aliyesajiliwa majira ya joto, Rasmus Hojlund kwa kiwango kikubwa msimu huu, aliyefunga bao moja katika mechi tisa, na hali yake Old Trafford ni ngumu kwa kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN, United walikuwa tayari kumwacha Martial aondoke msimu wa joto, lakini ofa pekee ya kweli iliyopokelewa ilitoka kwa Ligi Kuu ya Saudia na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alikataa nafasi ya kuingia kwenye mazungumzo juu ya kuhama.

United wameweka wazi chaguo zao kwa Martial, kutegemeana na jinsi atakavyocheza kati ya sasa na mwisho wa msimu.

United, hata hivyo, wanatazamiwa kuchukua mtazamo tofauti kwa walinzi Wan-Bissaka na Lindelöf.

Wan-Bissaka ameshinda tena nafasi yake katika timu ya Erik ten Hag baada ya mwanzo mgumu chini ya Mholanzi huyo.

Mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, lakini United wana fursa ya kuuongeza kwa mwaka mmoja zaidi hadi 2025.

Klabu hiyo imepanga kutekeleza chaguo hilo kabla ya mwisho wa mwaka huku pia ikifungua mazungumzo kuhusu mkataba mpya wa muda mrefu.

United wako katika hali sawa kwa Lindelöf, ambaye ana mkataba hadi majira ya joto pamoja na chaguo la kuongeza mwaka mmoja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Sweden amefanya vya kutosha kumshawishi Ten Hag kuwa ana hatima ya kuishi Old Trafford na klabu iko tayari kuamsha nyongeza yake hadi 2025.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,161,7
MECHI KALI
NETHERLANDS
VERSUS
FRANCE
1 | 3.06
X | 3.43
2 | 2.26
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LUKAKU AMTAKA COURTOIS KUREJEA KIKOSINI UBELGIJI

**VIENNA, Austria**

NAHODHA wa Ubelgiji, Romelu Lukaku amesema atamkaribisha Thibaut Courtois kurejea katika timu hiyo kwa mikono miwili baada ya mlinda mlango huyo kutangaza kustaafu kukichezea kikosi hicho Juni, mwaka huu.

Akiwa amevuliwa unahodha, Courtois alikataa kucheza mechi ya kufuzu michuano ya Ulaya dhidi ya Estonia iliyochezwa Juni, kwa mujibu wa Kocha, Domenico Tedesco ambaye wiki hii alisema tangu wakati huo hajawasiliana na mlinda mlango huyo wa Real Madrid.

Courtois alipasuka mishipa ya goti na kufanyiwa upasuaji Agosti, na kumweka nje kwa muda wa miezi sita, lakini mapema wiki hii beki wa pembeni wa Ubelgiji, Timothy Castagne alisema hafikirii Courtois anaweza kurejea kikosini bila maelezo yoyote.


Hata hivyo, Lukaku, alitoa maoni tofauti juu la Courtois kurejea kwenye kikosi hicho.

"Namaanisha kutoka moyoni mwangu: lazima tuweke kile kilichotokea nyuma yetu," alisema Lukaku akiwaambia waandishi wa habari wakati Ubelgiji ikijiandaa kwa mechi ya kufuzu dhidi ya Austria itakayopigwa mjini Vienna leo.

"Siku Thibaut akiamua kurejea atarudi tu, itatokea hivyo bado atakuwa wa thamani kubwa. Thibaut atajijibu mwenyewe kwenye chumba cha kubadilishia nguo.

"Tunahitaji kuyaweka sawa mambo hayo. Kupona kwaThibaut ndilo jambo muhimu zaidi sasa, na akirejea, nitakuwa wa kwanza kumkaribisha kwa mikono miwili."

Lukaku alichaguliwa mbele ya Courtois kama nahodha Juni, akisimama badala ya Kevin De Bruyne ambaye ni majeruhi.



# Chelsea wakomaa na Osimhen

**LONDON, England**

CHELSEA wamemwongeza mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen kwenye orodha ya wachezaji wanaowalenga wakati wa dirisha dogo la Januari, kwa mujibu wa ESPN.

Chelsea wanatafuta mshambuliaji wa kati na tayari wanamfuatilia mchezaji wa Brentford, Ivan Toney, ambaye pia anavutiwa na Arsenal kama ESPN ilivyoripoti Septemba 26, mwaka huu.

Osimhen amejijengea sifa ya kuwa mmoja wa washambuliaji wa kufurahisha zaidi barani Ulaya baada ya kufunga mabao 26 katika mechi 32 za Ligi Kuu Italia msimu uliopita huku Napoli ikitwaa taji lao la kwanza la Serie A tangu mwaka 1990.

Kiwango hicho kizuri -- ambacho kimeendelea hadi msimu huu kwa mabao sita kutoka mechi 10 -- kimepelekea Napoli kuweka dau la Osimhen hadi pauni milioni 120, ambayo ni karibu pauni milioni 40 zaidi ya thamani ya Toney.

Chelsea wanatarajia Christopher Nkunku, aliyesajiliwa kwa dau la pauni milioni 52 kutoka RB Leipzig -- kupatikana mapema mwaka mpya baada ya upasuaji wa goti kwa kuongoza safu ya ushambuliaji pamoja na Nicolas Jackson na Armando Broja.



95,478/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/10/23 | 19:30 | Sporting Gijon vs Real Zaragoza | 2.12 | 3.00 | 3.65 |
| 02. 14/10/23 | 19:30 | FC Cartagena vs Racing Santander | 2.24 | 3.05 | 3.25 |
| 03. 14/10/23 | 21:45 | Hungary vs Serbia | 2.42 | 3.05 | 2.65 |
| 04. 14/10/23 | 23:00 | Ituano vs CR Brasil | 2.30 | 2.95 | 3.25 |
| 05. 14/10/23 | 23:00 | Detroit City vs Pittsburgh Riverhounds | 2.65 | 3.40 | 2.25 |
| 06. 15/10/23 | 00:00 | Deportivo Pereira vs La Equidad | 2.15 | 3.05 | 3.05 |
| 07. 15/10/23 | 02:05 | Alebrijes de Oaxaca vs Cancun | 2.21 | 3.20 | 2.85 |
| 08. 15/10/23 | 02:10 | Atletico Nacional vs Independiente Medellin | 2.13 | 3.10 | 3.05 |
| 09. 15/10/23 | 03:00 | Cuiaba vs Cruzeiro | 2.35 | 3.05 | 3.05 |
| 10. 15/10/23 | 05:00 | Monterey Bay vs Orange County | 2.16 | 3.40 | 2.75 |
| 11. 15/10/23 | 05:30 | Las Vegas Lights vs San Diego Loyal | 2.85 | 3.40 | 2.11 |
| 12. 15/10/23 | 05:30 | LA Galaxy vs Real Salt Lake | 2.25 | 3.65 | 2.50 |
| 13. 15/10/23 | 08:00 | Osaka vs Gifu | 2.75 | 2.90 | 2.43 |
| 14. 15/10/23 | 17:15 | Eldense vs Elche | 3.30 | 3.05 | 2.22 |
| 15. 15/10/23 | 17:30 | Preussen Munster vs 1860 Munich | 2.17 | 3.35 | 2.75 |
| 16. 15/10/23 | 21:30 | CA Estudiantes vs Tristan Suarez | 2.20 | 3.30 | 3.10 |
| 17. 15/10/23 | 21:45 | Ponte Preta vs AC Goianiense | 3.10 | 2.90 | 2.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 13/10/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:35 | 5486 | Japan vs Canada | 1.58 | 4.06 | 5.49 |
| 14:00 | 3795 | South Korea vs Tunisia | 1.88 | 3.49 | 4.13 |
| 15:00 | 4575 | Hambericho Durame vs Saint George FC | 8.60 | 4.20 | 1.31 |
| 16:00 | 2185 | Malaysia vs India | 1.71 | 3.64 | 4.97 |
| 16:00 | 3612 | ND Gorica vs Tabor Sezana | 1.18 | 5.88 | 11.15 |
| 17:00 | 1694 | NRB Teleghma vs Ib Khemis El Khechna | 2.75 | 3.00 | 2.48 |
| 17:00 | 2029 | ZR Temouchent vs Skaf Khemis Miliana | 1.57 | 3.73 | 5.11 |
| 17:00 | 2405 | ASM Oran vs RC Kouba | 2.18 | 3.00 | 3.25 |
| 17:00 | 2525 | USM Annaba vs CA Batna | 2.03 | 2.90 | 3.81 |
| 17:00 | 3573 | Ol. Medea vs NA Hussein Dey | 1.74 | 3.36 | 4.38 |
| 18:00 | 2627 | FK Babrungas Plunge vs Lietava Jonava | 1.26 | 5.20 | 7.40 |
| 18:00 | 2843 | Iraq vs Qatar | 3.26 | 3.21 | 2.26 |
| 18:00 | 5708 | Fasil Kenema vs Ethiopian Medhin | 2.32 | 3.02 | 2.96 |
| 18:30 | 4480 | Societe Omnisport vs Racing Club Dabidjan | 1.96 | 3.20 | 3.61 |
| 19:00 | 4092 | Saudi Arabia vs Nigeria | 4.01 | 3.48 | 1.91 |
| 19:00 | 4658 | New Zealand vs DR Congo | 3.63 | 3.21 | 2.11 |
| 19:00 | 4865 | South Africa vs Eswatini | 1.43 | 4.44 | 7.41 |
| 19:00 | 5402 | FC Zurich II vs FC Bulle | 1.69 | 4.00 | 3.60 |
| 19:00 | 5694 | Estonia vs Azerbaijan | 2.33 | 3.02 | 3.34 |
| 19:45 | 5644 | SC Gleisdorf vs WSC Hertha | 2.85 | 3.70 | 2.01 |
| 20:00 | 2310 | Skra Czestochowa vs Wisla Pulawy | 2.39 | 3.21 | 2.70 |
| 20:00 | 2616 | Spartak Myjava vs Slovan Bratislava B | 1.68 | 3.92 | 4.02 |
| 20:00 | 2745 | Atsv 1898 Erlangen vs ASV Cham | 3.70 | 3.80 | 1.70 |
| 20:00 | 2968 | Borussia Dortmund II vs RW Essen | 2.13 | 3.38 | 3.17 |
| 20:00 | 3185 | Koblenz vs Homburg | 8.12 | 5.48 | 1.26 |
| 20:00 | 3610 | Lindome Gif vs Qviding Fif | 1.89 | 3.80 | 3.05 |
| 20:00 | 5438 | Memmingen vs Eintracht Bamberg | 1.90 | 3.61 | 3.36 |
| 20:30 | 3368 | Fortuna Koln vs ROT Weiss Ahlen | 1.22 | 5.70 | 9.37 |
| 20:30 | 3994 | Victoria Hamburg vs Etsv Hamburg | 2.70 | 3.55 | 2.13 |
| 20:30 | 4486 | Wiedenbruck vs SV Rodinghausen | 3.52 | 3.72 | 1.83 |
| 21:00 | 1370 | Jordan vs Iran | 4.01 | 3.38 | 1.94 |
| 21:45 | 1669 | Glenavon vs Cliftonville Belfast | 6.45 | 4.54 | 1.36 |
| 21:45 | 2541 | Austria vs Belgium | 2.79 | 3.26 | 2.53 |
| 21:45 | 3389 | England vs Australia | 1.24 | 5.94 | 11.67 |
| 21:45 | 3557 | Dungannon Swifts vs Larne | 6.66 | 4.64 | 1.34 |
| 21:45 | 4339 | Crusaders Belfast vs Ballymena Utd | 1.21 | 5.64 | 9.47 |
| 21:45 | 4429 | Carrick Rangers vs Linfield Belfast | 7.47 | 4.95 | 1.29 |
| 21:45 | 4586 | Fiorenzuola vs Legnago | 2.67 | 3.04 | 2.73 |
| 21:45 | 4621 | Netherlands vs France | 3.06 | 3.43 | 2.26 |
| 21:45 | 4774 | Novara vs Arzignanochiampo | 2.39 | 3.04 | 3.09 |
| 21:45 | 4977 | Liechtenstein vs Bosnia and Herzegovina | 22.17 | 8.24 | 1.12 |
| 21:45 | 5116 | Portugal vs Slovakia | 1.27 | 5.52 | 10.62 |
| 21:45 | 5235 | Glentoran Belfast vs Loughgall | 1.23 | 5.23 | 9.65 |
| 21:45 | 5395 | Albinoleffe vs Vecomp Verona | 3.03 | 3.08 | 2.40 |
| 21:45 | 5434 | Ireland vs Greece | 2.49 | 3.01 | 3.07 |
| 21:45 | 5570 | Newry City AFC vs Coleraine FC | 4.76 | 4.05 | 1.53 |
| 21:45 | 5724 | Iceland vs Luxembourg | 1.87 | 3.44 | 4.24 |
| 22:00 | 2302 | Real Oviedo vs Albacete Balompie | 2.23 | 2.97 | 3.27 |
| 22:00 | 2849 | CA Fenix vs Plaza Colonia CD | 1.96 | 3.07 | 3.63 |
| 22:30 | 4986 | Saint Vincent and the Grenadines vs French Guiana | 2.85 | 3.36 | 2.21 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# STARS YAELEKEA SAUDI ARABIA KUIVAA SUDAN

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka la Taifa (Taifa Stars) kinaondoka nchini leo kuelekea Saudi Arabia kwa ajili ya mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Sudan, imefahamika.

Taifa Stars itakutana na Sudan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa ambayo itachezwa keshokutwa nchini Saudi Arabia.

Mechi hiyo ya kirafiki itachezwa katika siku inayotambuliwa na kalenda ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo alisema wachezaji wa timu hiyo waliingia kambini juzi kwa ajili ya kujiandaa na mechi hiyo yenye lengo la kuwaimarisha kuelekea michuano mbalimbali iliyoko mbele yao.

Ndimbo alisema, baadhi ya wachezaji wa timu hiyo ambao wako katika majukumu ya klabu zao watatungana na kikosi hicho nchini Saudi Arabia. Alisema maandalizi yote ya safari ya kikosi hicho kinachoongozwa na Kocha Mkuu, Adel Amrouch yamekamilika na kuongeza mechi nyingine ya kirafiki iliyotarajiwa kuchezwa dhidi ya Libya haitafanyika tena.

"Ni kweli awali tulipanga kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Sudan, mchezo wa pili dhidi ya Libya hautachezwa, wachezaji wanaocheza soka la kulipwa ambao hawapo kwenye kikosi hapa nchini, watajiunga na timu moja kwa moja nchini Saudia," alisema Ndimbo.

Taifa Stars imefuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mapema mwakani huko Ivory Coast.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Sudan itakayochezwa keshokutwa. **PICHA: TFF**

# Azam yairejesha Yanga 'darasani'

INATOKA UK. 24

ratiba itaendelea kuwa hivyo, " alisema Harrison.

Meneja huyo aliongeza Yanga inaamini hakuna mechi rahisi katika ligi hiyo na ndio maana wanaendelea kujiimarisha na kuwa tayari kwa ushindani.

Wachezaji wa Yanga walioitwa katika kikosi cha Tanzania (Taifa Stars) ni pamoja na Metacha Mnata, Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Hamad 'Bacca', Nickson Kibabage, Dickson Job, Mudathir Yahaya na Clement Mzize wakati Khalid Aucho ameenda kujiunga na timu yake ya Uganda.

Mshambuliaji, Stephane Aziz Ki ameitwa katika kikosi cha Burkina Faso na kipa namba moja, Djigui Diarra amekwenda kuitumikia Mali.

Mapema wiki hii Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema kwa sasa anaifuatilia Azam FC kupitia video mbalimbali kwa lengo la kuisoma na ili kuyafanyia kazi mazuri na madhaifu yao.

Yanga inakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 12, juu yake ikiwa Azam FC yenye pointi 13 na Simba ikiwa kileleni na pointi zake 15 kibindoni.

# Simba: Hatutawaangusha

INATOKA UK. 24

maalum ya mashindano ya AFL ambayo ni mara ya kwanza yanafanyika na kuzinduliwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikicheza dhidi ya Al Ahly," alisema bosi huyo.

Simba itaingia katika michuano hiyo ikiwa ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushinda mechi zake tano ilizocheza ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 13 huku mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 12 ikifuatiwa.

Michezo
Ijumaa Oktoba 13, 2023
Nipashe

United haijaamua hatima ya Martial UKURASA 21





Wachezaji wa Simba wakiwa na jezi mpya zitakazotumika katika michuano ya Africa Football League (AFL) ambayo uzinduzi wake utafanyika Oktoba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# SIMBA: HATUTAWAANGUSHA

## ●●●Yaahidi furaha michuano ya AFL ikizindua uzi mpya...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikizindua rasmi jezi mpya zitakazotumika katika mashindano ya Africa Football League, uongozi wa Wekundu wa Msimbazi umetamba kikosi chao ni bora na kimestahili kuwamo kwenye michuano hiyo na inaahidi haitawaangusha.

Simba itawakaribisha Al Ahly kutoka Misri katika mechi ya ufunguzi ya michuano hiyo itakayochezwa Oktoba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kupitia mzabuni klabu hiyo, Kampuni ya Sandaland Fashion Wear, Simba jana ilitambulisha rasmi jezi mpya (nyekundu na nyeupe), watakazovaa katika mashindano hayo yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa jezi hizo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema lengo lao ni kuona timu inakuwa na mwonekano mpya katika mashindano hayo mapya ambayo yanafanyika kwa mara ya kwanza na timu yao imepata nafasi ya kushiriki.

Try Again alisema michuano hiyo ni mikubwa na Simba imefanikiwa kuwa katika timu nane bora, hivyo mzabuni wao aliamua kuipa heshima timu kwa kupata mwonekano mpya.

"Sandaland alinihakikishia jezi hizi zinaenda kupiga tena, baada ya uzinduzi huu jezi zimeanza kuuzwa, naomba mashabiki kununua ili kuzivaa na kuanza kupendeza.

Naomba mashabiki wanunue na wavae kwa sababu kuna wageni wengi wanakuja na kuona hapa Tanzania hakuna klabu nyingine zaidi ya Simba," alisema Try Again.

Alimwakikishia mzabuni huyo Simba haitawaangusha na dhamira yao ni kuendelea kuwapa furaha mashabiki huku wakiwa wamependeza kwa kuvaa jezi mpya katika kila michuano iliyopo mbele yao.

Aliwataka na kuwakumbusha wanachama wao kununua tiketi mapema kama utaratibu wao ulivyo ili kwenda kuujaza uwanja siku hiyo kama inavyokuwa katika Tamasha la Simba Day.

Naye Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu aliwashukuru wadhamini wao kwa kufanikisha jezi hizo mpya zinapatikana na kuongeza tukio hilo ni zawadi kwa wanachama na mashabiki wao.

Mangungu alisema Simba iko imara na kamwe haitayumbishwa na maneno yanayosemwa na baadhi ya watu kuhusu nafasi ya wao kushiriki katika mashindano hayo.

"Tutashughulika nao wale wote wanaoleta propaganda ya kuiumiza Simba, hatutakubali kuona mtu anaichafua klabu, nawaomba wanasimba kuwa pamoja na kushirikiana na viongozi katika kuifanya Simba inakuwa imara," Mangungu alisema.

Mkurugenzi wa Sandaland Fashion Wear, Yusuf Omary alisema kwa sababu Simba imepiga hatua kubwa, kampuni yake iliamua kutengeneza jezi bora zaidi zitakazotumika katika mechi hiyo dhidi ya Al Ahly.

"Jezi hizo ni bora na tunazindua leo (jana), zitavaliwa rasmi katika siku hiyo

UKURASA. 23

# Azam yairejesha Yanga 'darasani'

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi, Yanga wameanza mazoezi rasmi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC inayotarajiwa kuchezwa Oktoba 25, mwaka huu.

Wachezaji wa Yanga ambao hawajaitwa katika timu za taifa walirejea mazoezini juzi na lengo likiwa ni kujifua kuelekea mechi hiyo inayotarajiwa kuwa ngumu na yenye ushindani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Yanga, Walter Harrison alisema tayari programu ya mazoezi ya uwanjani na 'darasani' kuelekea mechi hiyo imeanza na wachezaji wengine watakaporejea, wataendelea ili kutengeneza muunganiko.

Harrison alisema Yanga inafahamu mechi hiyo ni muhimu kwao katika kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi huku ikiamini nyota waliokwenda katika timu za taifa watarejea wakiwa imara.

"Kuna wachezaji walioondoka kwenda kuzitumikia timu zao za taifa, kuna wachezaji wa Tanzania, Mali, Uganda, Burkina Faso, wote wameenda kuziwakilisha nchi zao, lakini wale ambao hawajaitwa kwenye timu yoyote wameshaanza mazoezi kujiandaa na mchezo utakaofuata dhidi ya Azam kama

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >